SportPesa
TZS. 499,059,740
CHEZA USHINDE JACKPOT
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Azua** taharuki kwa madai ya kujifungua mnyama karunguyeye

UKURASA 3




UKURASA 11

Nipashe
Ijumaa Septemba 17, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580706
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Rugemalira: Sina kinyongo na mtu

**Ni** baada ya kuachiwa huru, vilio vya furaha vyatanda, mwenyewe aanzia kanisani...

*Endelea ukurasa 2*



Mzee Rugemalira, akiwa mwenye furaha na familia yake, baada ya kuachiliwa huru katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jana. **PICHA: MTANDAO**



James Rugemalira (kulia), akiwa amechuchumaa siku alipofikishwa kwa mara ya kwanza katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Juni 19, 2017. **PICHA: MAKTABA**



# Yalivyokuwa mabishano saa tatu kesi ya Mbowe

UKURASA 2




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna (kulia), akimkabidhi Mweka Hazina Mkuu wa NMB, Aziz Chacha, moja kati ya tuzo nne za kimataifa ilizoshinda benki hiyo zilizotolewa na majarida yanayoaminiwa na taasisi za kifedha duniani, jijini Dar es Salaam jana. Katikati ni Ofisa Mkuu wa Fedha wa benki hiyo, Juma Kimori. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Msekwa asema Rais Samia ameeleweka

UKURASA 3

MICHEZO **GOMEZ: SIMBA IPO TAYARI KWA MIKIKI** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Rugemalira: Sina kinyongo na mtu

**Na Waandishi Wetu**

VILIO vya furaha vilitawala jana kwenye viunga vya Mahakama ya Hakimu Mkazi Dar es Salaam kutoka kwa wanafamilia na ndugu baada ya kuachiwa huru kwa mfanyabiashara James Rugemalira aliyekuwa anakabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi.

Hatua hiyo ilifikiwa jana baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuwasilisha hati ya Nole chini ya kifungu cha 91(1) kwamba hana nia ya kuendelea na mshtakiwa Rugemalira.

Kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Huruma Shaidi. Mshtakiwa huyo alikuwa mahabusu gerezani kwa takriban miaka minne na miezi mitatu tangu Juni 19, 2017, alipopandishwa kizimbani kusomewa mashtaka dhidi yake.

Mapema jana, Wakili wa Serikali, Grace Mwanga, alidai mahakamani huko kwamba kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa.

Hata hivyo, alidai DPP ametoa hati ya Nole chini ya kifungu cha 91(1) cha Mwenendo wa Makosa ya Jinai kwamba hana nia ya kuendelea na kesi hiyo dhidi ya Rugemalira.

"DPP hana nia ya kuendelea na kesi hii dhidi ya Rugemalira, tunaiomba mahakama imwachie," alidai Wakili Mwanga.

Hakimu Shaidi alisema kwa kuwa Jamhuri hawana nia ya kuendelea na kesi hiyo, mahakama inamwachia huru chini ya Kifungu cha 91(1).

Mbali na Rugemalira, mshtakiwa mwingine katika kesi hiyo ni Joseph Mwakandege ambaye kesi yake itatajwa Septemba 23, mwaka huu.

Awali, Rugemalira aliwasilisha hoja kuomba kuondolewa na DPP katika kesi ya uhujumu uchumi.

Alidai mahakamani kuwa aliandika barua kwa Kamishna wa TRA kupitia mjumbe wa Taasisi ya Kuzuia na Kupamba na Rushwa (TAKUKURU) aliyetembelea gerezani akielezea jinsi Benki ya Standard Chartered Hong Kong inavyokwepa kodi na kudai kuwa wanaostahili kujumuishwa kwenye kesi ni benki hiyo na sio yeye.

Pia alidai aliandika notisi kwa taasisi tisa ikiwamo Usalama wa Taifa (TISS) akitaka DPP awasilishe hati ya kuachiwa kwake na asipofanya hivyo, yeye atawasilisha hoja ya kuiomba mahakama imwondoe katika kesi hiyo.

Katika kesi ya msingi ya uhujumu uchumi namba 27/2017, Makandege anakabiliwa na mashtaka matano likiwamo la kuisababishia serikali hasara ya Dola za Marekani 980,000, pia yapo ya utakatishaji wa fedha.

Mshtakiwa huyo alisomewa mashtaka hayo Desemba 20, 2019 baada ya kuunganishwa na washtakiwa Mkurugenzi wa Kampuni ya Kufua Umeme ya IPTL, HerbinderSeth na Rugemalira katika kesi hiyo ya uhujumu uchumi.

Makandege anadaiwa kuwa, kati ya Oktoba 18, 2011 na Machi 19, 2014 katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam, Kenya, Afrika Kusini na India, akiwa na wenzake walikula njama ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Katika kesi hiyo, Rugemalira alikuwa anakabiliwa na mashtaka 12, likiwamo la utakatishaji fedha na kusababisha hasara ya Dola za Marekani 22,198,544.6 na Sh. 309,461,300,158.27 (Sh. bilioni 309.5).

**'SINA KINYONGO NA MTU'**

Baada ya kuachiwa huru, Rugemalira aliongozana na baadhi ya ndugu na jamaa zake hadi Kanisa Katoliki Makongo Juu Parokia ya Bikra Maria Mama wa Rozari Takatifu kulikofanyika ibada ya shukrani ambalo ni muumini wake.

Wakati wa ibada hiyo, Paroko wa Kanisa hilo, Joseph Masenge, alimtaka Rugemalira kusamehe, Rugemalira akijibu kuwa 'sina kinyongo na mtu, nimewasamehe wote'.

Baada ya kumalizika kwa ibada hiyo ya shukrani, Rugemalira alitembezwa kuangalia mandhari ya nje ya kanisa hilo zikiwamo nyumba za watumishi wake, akieleza kufurahishwa na ujenzi uliofanyika.

Nipashe ilizuru nyumbani kwa Rugemalira kwa nia ya kuzungumza na mfanyabiashara huyo, lakini walinzi walizuia kwa maelezo kwamba maagizo waliyopewa ni kuhakikisha hakuna mtu anayeruhusiwa kuingia ndani ya nyumba hiyo kwa jana, vinginevyo awe mwanafamilia.

**KAULI YA LHRC**

Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, akizungumzia kuachiwa huru kwa mfanyabiashara huyo, alisema kuna mchanganyiko wa furaha na huzuni katika tukio hilo, akifafanua kwamba furaha iko kwenye kuachiwa huru baada ya kukaa gerezani kwa miaka mingi na huzuni iko katika kusota miaka mingi gerezani bila dhamana na sasa DPP anasema hana mpango wa kuendelea na kesi.

"Kwa miaka mingi amesota, halafu DPP anasema hana sababu ya kuendelea na kesi. Kwa nini asingeona hivyo mwezi wa kwanza au miezi sita ya mwanzo?" Alihoji.

Kwa mujibu wa Henga, sheria ya jinai ina dosari kwa kuwa mtuhumiwa anasota kwa muda mrefu kwa kusingizio cha upelelezi haujakamilika, hali inayomfanya kuwa kama mfungwa kwa miaka mingi bila kosa lolote.

Alinyoshea kidole sheria ya kumlinda DPP na wapelelezi kwa kuwa aliyetendewa hayo hawezi kushtaki kudai fidia kwa muda na rasilimali alizopoteza.

**●Imeandaliwa na Hellen Mwango, Romana Mallya na Salome Kitomari**



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe (kulia), akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza, baada ya kufikishwa katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, mkoani Dar es Salaam jana, kusikiliza kesi ya ugaidi inayomkabili. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Yalivyokuwa mabishano saa tatu kesi ya Mbowe

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi jana ilikwama kwa saa tatu kuendelea kusikiliza kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, na wenzake watatu kwa sababu ya mabishano yaliyoibuka baada ya kuruhusiwa wasikilizaji wachache kuingia katika chumba cha mahakama na bila simu.

Mabishano hayo yaliibuka jana saa nne asubuhi ulipotangazwa utaratibu mpya ambao uliuza tafrani kwa wasikilizaji wa kesi wakiwamo wanachama wa CHADEMA waliosimama getini wakitaka kuingia.

Tangazo lililotolewa na mahakama lilisisitiza watakaoruhusiwa kuingia ni waandishi wa habari 10, mawakili 20, kundi maalum watatu, viongozi wa kisiasa watano, askari polisi watano, ndugu watano na wapigapicha ambao waliruhusiwa kuingia kupiga picha na kutoka.

Wasikilizaji waligoma kuacha simu getini hali iliyosababisha kuibuka kwa mvutano wa muda mrefu.

Akizungumzia sintofahamu hiyo, Naibu Msajili wa Mahakama hiyo, Magdalena Ntandu, alisema sababu ya kuweka utaratibu ni vikwazo vilivyojitokeza ikiwamo mahakama kuzidiwa idadi kubwa ya watu, ambalo ni tatizo kiafya.

Alibainisha mahakama ina uwezo wa kuketisha watu 45, lakini idadi ya wanaoingia katika kesi hiyo ni kubwa hadi viyoyozi vinashindwa kufanya kazi, hivyo waliona haja ya kuweka utaratibu kuingia wawakilishi kutoka kila kundi.

"Lengo la kuamua kuingia wawakilishi ni suala la kiafya, watu wanaingia na simu wanarekodi mwenendo wa kesi na kurusha katika mitandao wakati wanaoruhusiwa kusambaza habari ni waandishi wa habari ambao wana miiko.

"Simu zinaita na kusababisha kelele, watu wote wanatakiwa kuzima simu, simu ikiita inaondoa utulivu, yanayorekodiwa na kurushwa katika mitandao hayana uhalisia, yanapotosha, kazi ya kuchambua ushahidi ni kazi ya mahakama," alisema.

Msajili Magdalena alisema walijadiliana na mawakili wa pande zote mbili wakafikia mwafaka wa simu zote zizimwe na kama watu hawawezi kuzima, wasirekodi mwenendo wa shauri.

Baada ya kufikia mwafaka saa saba mchana, pande zote mbili ziliingia mahakamani kwa utaratibu uliowekwa na kesi iliendelea kwa Upande wa Jamhuri kumalizia kumhoji Kamishna Msaidizi wa Polisi, Ramadhani Kingai, kulingana na ushahidi wake katika kesi ndogo iliyoanza kusikilizwa jana.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Robert Kidando, shahidi alidai haikuwa lazima kuleta mahakamani 'kidaftari' kidogo alichokuwa akiandika kumbukumbu wakati wa kuwakamata washtakiwa.

ACP Kingai alidai mshtakiwa Adamu Kasekwa alimfahamisha tatizo la afya ya akili na alimwambia alipata matibabu Mbeya na kwa wakati huo alikuwa sawa.

Wakili Kidando alimaliza kumhoji na aliifahamisha mahakama kuwa walikuwa na shahidi mmoja kati ya saba wanaotakiwa kutoa ushahidi katika kesi ndogo.

Kidando alidai mashahidi wengine wanatoka nje ya Dar es Salaam, hivyo aliomba kesi iahirishwe hadi leo, waendelee na shahidi wa pili.

Upande wa Utetezi haukuwa na pingamizi, mahakama iliahirisha kesi hiyo hadi leo saa nne asubuhi.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, komandoo, Halfani Bwire, Adam Kasekwa, maarufu Adamo na Mohamed Ling'wenya, ambao wanakabiliwa na mashtaka sita.

# Msekwa: Samia ameeleweka

**Na Beatrice Shayo**



SPIKA mstaafu Pius Msekwa (pichani) amesema kauli ya Rais Samia Hassan Suluhu kupata Rais mwanamke katika Uchaguzi Mkuu ujao ni jambo ambalo lipo wazi na inaeleweka.

Juzi Rais Samia wakati wa maadhimisho ya Siku ya Demokrasia Duniani, alisema: "Nataka niwaambie wanawake wenzangu kwamba bado hatujaweka Rais mwanamke nchini, tumepata Rais mwanamke kwa kudra za Mungu na Katiba. Niseme tu Rais mwanamke tutamweka mwaka 2025."

Nipashe ilizungumza na Spika Msekwa jana kwa njia ya simu kupata maoni kuhusu kauli hiyo ya Rais Samia.

Msekwa alihoji: "Kuna mtu yeyote ambaye hajaelewa kauli hiyo? Hii kauli kuna mtu hakuielewa? Maoni ya mzee ni pale jambo kama halijaeleweka, unasema mzee hebu tusaidie. Sasa hili jambo lipo wazi, kwani wewe hukumwelewa?

"Kwa uzoefu wangu labda kama jambo halikueleweka," Msekwa alisema.

Alipoulizwa kama kauli hiyo haitaleta ukakasi katika vikao vya uteuzi wa wagombea ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Msekwa alisema haoni shida huku akisisitiza yeye halitamsumbua kwa kuwa ni mstaafu.

# Azua taharuki akidai kujifungua mnyama karunguyeye

**Na Happy Severine,** BARIADI

KATIKA hali isiyo ya kawaida, mkazi wa mtaa wa Butiama, mji wa Bariadi Regina Frednand (46), amedai kujifungua mnyama aina ya karunguyeye na kuzua taharuki kwenye eneo hilo.

Akiongea na waandishi wa habari waliofika nyumbani kwake jana na kukuta umati wa watu uliofika kushuhudia tukio hilo, mama huyo alisema kuwa tukio hilo lilitokea Jumapili iliyopita Agosti 12, 2021.

Regina alisema majira ya saa 1:10 asubuhi wakati akijiandaa kwenda kwenye ibada ya kwanza kanisani, gafla alijisikia maumivu makali tumboni na ndipo akaelekea chooni kujisaidia.

"Baada ya kufika chooni huku nikiwa na maumivu makali, haja ambayo nilikuwa nikisia haikutoka...cha kushangaza nilisikia maumivu makali sehemu za siri na kuhisi kuna kitu kinaning'ata," alisema Regina.

"Kadiri maumivu yalivyoongezeka nikajisikia kusukuma ndipo kikatoka kitu ambacho sikukielewa...nikapiga kelele kuomba msaada kwa watoto wangu ambao naishi nao hapa, baada ya kufika walikitazama na kubaini kuwa alikuwa panyabuku, baadaye wakakimwagia maji ya baraka ndipo kilipogeuka na kuwa mnyama aina ya karunguyeye," alieleza Regina.

Alipoulizwa kama alikuwa mjamzito, Regina alikiri kuwa na ujauzito wa miezi mitano ambao aliupima mwenyewe nyumbani kwa kutumia kipimo cha mkono alichonunua duka la dawa.

Hata hivyo, alisema hakuwahi kwenda kliniki kwa madai kuwa alikuwa anasubiri ujauzito ufikishe miezi sita ndipo tukio hilo lilitokea kabla ya kuanza kliniki.

"Baada ya tukio kutokea nikawaita ndugu na wazazi wangu waje kushuhudia kwa sababu lilikuwa la ajabu, siku ya Jumatatu nilijisikia vibaya nikaamua kwenda hospitali ya Wilaya Somanda kwa ajili ya vipimo," alisema Regina.

"Nilifika hospitali nikawaeleza tukio zima, kisha nikafanyiwa kipimo cha mionzi na majibu ya kipimo hicho yalionyesha hapakuwa na kitu chochote tumboni," alisema Regina.

Mwanamke huyo alisema kuwa baada ya kutoka hospitali waliendelea na maombi nyumbani hapo huku wakiwashirikisha viongozi wa dini na mnyama huyo alichomwa moto na viongozi wa dini.

Mama mzazi wa Regina Maimuna Fransic, alisema baada ya kupigiwa simu na mtoto wake alifika nyumbani hapo na kukiri kuwa alikuta amejifungua mnyama huyo na kubaki wanastaajabu.

"Kila mtu hapo ndani tulibaki tunashangaa hili jambo limetoka wapi, katika historia ya ukoo wetu halijawahi kutokea, mtoto wangu na mume wake wamekuwa wakiishi kwa kumtegemea Mungu," alisema Maimuna.

Hata hivyo, alipoulizwa kama mtoto wake alikuwa na ugomvi na mtu, alisema kuwa hakuwahi kusikia jambo hilo au ndoa yake kuwahi kuingiliwa na mtu mwingine.

Naye Paul Manyangu mmoja wa majirani nyumbani hapo, alisema alishiriki kumsaidia mama huyo baada ya kupiga kelele chooni na kushangaa kuona amejifungua mnyama.

"Tulibaki kila mtu na mshangao na kuogopa sana, lakini ndiyo hali halisi iliyojitokeza kila kitu tunamwachia Mungu yeye ndiye anajua nini kipo nyuma ya pazia, lakini kwa jinsi ambavyo tumeishi na hii familia ni watu wa kumtegemea Mungu sana," alisema Manyangu.

**Daktari.**

Mganga Mfadhiwi Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Bariadi (Somanda), Dk. Emmanuel Costanine, alikiri mama huyo kufika hospitalini hapo na kufanyiwa vipimo ambavyo vilionyesha hakuwa na ujauzito wala hakujifungua.

Dk. Costantine alisema kuwa walimfanyia vipimo viwili, cha kwanza ni kipimo mkono ambacho kilionyesha hakuwa na ujauzito wowote na kipimo cha pili ni Ultrasound ambacho kilionyesha tumboni hakukuwa na kitu chochote na wala hakujifungua," alisema Dk. Costantine.

**Polisi**

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Simiyu, ACP Richard Abwao alikiri jeshi hilo kupokea taarifa za tukio hilo na wanaendelea na uchunguzi zaidi ili kubaini ukweli wake ikiwamo kupata taarifa za kitaalamu kutoka kwa madaktari.


**Air Tanzania**
The Wings of Kilimanjaro

## TRAINING INSTITUTE

## KOZI YA WAFANYAKAZI NDANI YA NDEGE (CABIN CREW)

Chuo Cha Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL Training Institute ) kina furaha kuwatangazia watanzania wote kuwa kwa mara nyingine kitaendesha kozi ya wafanyakazi ndani ya ndege (Cabin Crew ) kuanzia tarehe 18/10/2021. Kozi hii ni ya muda wa miezi mitatu (03), chuo kipo uwanja wa ndege wa kimataifa wa Julius Nyerere-Dar es salaam (JNIA) terminal one kwenye jengo la utawala la ATCL karibu kabisa na kituo cha polisi uwanja wa ndege. Chuo kinakaribisha maombi ya kujiunga na kozi hii kwa wenye sifa zilizoainishwa hapo chini. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 24/09/2021.

**Sifa za mwombaji.**

i. Awe na umri kuanzia miaka 18 hadi miaka 25
ii. Awe timamu kiakili, kimaumbile na urefu kuanzia futi 5"4 na kuendelea
iii. Elimu sio chini kidato cha nne na ufaulu mzuri hasa masomo ya kiingereza, Jiografia na Historia (A,B,C,D)
iv. Aweze kuongea na kuandika kwa ufasaha lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Muombaji mwenye uelewa wa lugha zaidi ya hizi mbili kama Kiarabu, Kichina, Kihindi na Kifaransa atapewa kipaumbele.
v. Awe Mtanzania au raia wa kigeni mwenye vibali halali vinavyomruhusu kukaa au kusoma nchini.
vi. Asiwe na mchoro au tojo ( visible tattoo) kwenye sehemu za mwili zinazoonekana.

**Barua ya maombi iambatane na vitu vifuatavyo.**

i. Nakala za vyeti vya shule/chuo alikosoma
ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
iii. Picha mbili ndogo (passport size) na picha moja yenye kuonyesha umbo lote ukubwa wa 6x8
iv. Curriculum Vitae –CV
v. Kwa wageni, vibali vya kukaa au kusoma Tanzania

**Fomu ya Maombi ni bure.**
**Maombi yatumwe kwa:**
**Principal**
**ATCL Training Institute**
**Box no 543**
**Dar Es Salaam.**
**Email , training@airtanzania.co.tz**

**Mob: +255735787212 , Landline: +255222842543**
**ATCL TRAINING INSTITUTE.**




PO Box 123456 / Dar es Salaam, Tanzania
Tel: +254 20123456 / Fax +254 20123456 /email:info@airtanzania.com
website:www.airtanzania.com

216462101

HABARI KITAIFA

## Jela miaka 180 unyang'anyi wa kutumia silaha

**Na Halima Ikunji,** NZEGA

WATU sita wamehukumiwa kifungo cha jumla ya miaka 180 baada ya kupatikana na hatia ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

Akitoa hukumu hiyo jana katika Mahakama ya Wilaya ya Nzega, Hakimu Mkazi Mhere Mwita alisema kutokana na ushahidi uliotolewa, usiotia shaka, mahakama imeridhia na kuwatia hatiani watu hao ambao watatumikia kifungo cha miaka 30 jela kila mmoja.

Alisema hukumu hiyo itakuwa fundisho kwa watu wengine wenye nia mbaya kama hiyo ya kufanya uhalifu ambao kwa sasa haulipi.

Awali, Wakili wa Serikali, Jenipher Mandago, aliiambia mahakama hiyo kuwa Juni 17, 2020, watu hao wakiwa na silaha mbalimbali, walivamia maduka manne katika kata ya Tongi wilayani Nzega na kuiba vitu mbalimbali vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni mbili.

Wakili huyo wa serikali alitaja watu hao ambao walivamia na kufanya unyang'anyi huo ni Juma Ramadhani, Mathias Hashim, Joseph Andrea, Igoma Kapole na Godfrey Mikaeli,

Kutokana na tuhuma hizo, wakili huyo aliomba mahakama hiyo kutoa adhabu kali kwa watuhumiwa hao, ili iwe fundisho kwao na kwa watu wengine wenye tabia kama hizo.

Kabla ya hukumu, Hakimu Mwita alitoa nafasi ya utetezi kwa watu hao ambao wote kwa pamoja waliomba mahakama hiyo kuwapunguzia adhabu kutokana na kutegemewa na familia zao.

Hata hivyo, Hakimu Mwita hakuridhika na utetezi huo na kuwahukumu watu hao kutumikia kifungo hicho cha miaka 30 jela kwa kila mmoja.

# Mbarawa aibua madudu ujenzi mwendokasi

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amemtaka mkandarasi anayejenga barabara ya mwendokasi kutoka Kariakoo hadi Mbagala, kurudia kipande chini kilometa mbili kilichojengwa chini ya kiwango ndani ya miezi mitano.

Aidha, ameagiza makandarasi wanaofanya makosa kama hayo zaidi ya mara moja kunyimwa tenda zingine za serikali, ili kutoa funzo la kuacha kucheza na miradi ya umma.

Waziri Mbarawa alitoa agizo hilo jana, alipofanya ziara ya kukagua miradi ya ujenzi wa barabara za mkoani wa Dar es Salaam, zikiwamo ya Mbagala na Kimara hadi Kibaha.

"Ujenzi huu uko chini ya kiwango, naomba mkandarasi afumue kipande chote cha kilometa mbili na kujenga upya. Hapa kwa mtu wa kawaida unaweza kuona ni kitu cha kawaida, lakini baada ya magari kupita tatizo litazidi kuwa kubwa. Kama tusingeona, tungekuwa tumeliwa," alisema Prof. Mbarawa.

Alisema barabara hiyo inajengwa kwa awamu mbili ambayo ya kwanza inagharimu Sh. bilioni 217 na awamu ya pili kwa Sh. bilioni 45 na kwamba kazi inaenda vizuri.

Kuhusu makandarasi wanaofanya kazi chini ya kiwango, alisema wanyimwe tenda ili kuwajengea nidhani ya kufanya kazi kwa uadilifu.

"Mkandarasi akirudia kosa kama hili, akarudia tena maeneo mengine mawili, akileta maombi ya tenda tupilieni mbali maombi yake," alisema waziri.

Alisema serikali itanunua mitambo ya skana za kufanya ukaguzi wa barabara kwa ajili ya kubaini ubora baada ya kujengwa na kwamba ilishanunua mtambo mmoja wa kukagua barabara, lakini ulikaa muda mrefu bila kufanya kazi, hivyo wataongeza mingine na kugawa kanda zote nchini.

Akizungumzia mradi wa ujenzi wa barabara hiyo, Mtendaji Mkuu wa Tanroads, Mhandisi Rogatus Mativila, alisema awali mradi huo ulitakiwa kukamilika mwaka huu, lakini utakamilika Machi mwaka 2023.

Alisema ulikuwa ukamilike mwaka huu miezi 47 tangu ujenzi uanze 2018, lakini ulichelewa kwa sababu za kimenejimenti.

Alitaja sababu ya barabara kuharibika kabla ya kuanza kutumika, alisema mchanga uliotumika kujengea ulikuwa na udongo wa mfinyanzi ndio sababu ya kuanza kupata ufa na matobo madogo madogo.

Awali Waziri Mbarawa akikagua ujenzi wa barabara ya njia nane kuanzia Kimara hadi Kibaha yenye urefu wa Kilometa 19.2, alisema ujenzi huo unaogharimu Sh. bilioni 161, umefikia asilimia 94.

Aliwataka makandarasi kumaliza kazi zilizobaki ambazo ni ujenzi wa madaraja ya kuvukia abiria kituo cha Mbezi Luis na Kwa Yusuph, ufungaji wa taa za kuruhusu magari, ujenzi wa barabara ya kuingia kituo cha mabasi cha Magufuli na ujenzi wa kituo cha daladala Kibamba.



Mkurugenzi wa Masoko wa Kampuni ya kutengeneza bidhaa mbalimbali ya Rungu Max, Noel Lema, akiwaonyesha waandishi wa habari bidhaa feki ya wembe wenye nembo ya kampuni hiyo, baada ya kuikamata kwa mfanyabiashara, Stephen Njira, wakati wa operesheni iliyofanywa na maofisa wa Tume ya Ushindani (FCC), katika eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Aliyenaswa tuhuma za bidhaa bandia ajitetea kwa Kisukuma

**Na Mary Geofrey**

MFANYABIASHARA Steven Njira, aliyekamatwa akidaiwa kuuza bidhaa bandia, amejibu maswali ya waandishi wa habari kwa lugha ya Kisukuma, akidai hakijui vyema Kiswahili.

Katika operesheni dhidi ya bidhaa bandia iliyofanywa na Tume ya Ushindani (FCC) kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi jijini Dar es Salaam juzi, mfanyabiashara huyo baada ya kukamatwa akiwa na maboksi manne ya nyembe zinazodaiwa kuwa bandia, alijibu maswali kwa lugha ya Kisukuma alipozungumza na waandishi wa habari walioshiriki operesheni hiyo. Alidai kuwa maboksi hayo ni kati ya 10 aliyokuwa amenunua kwa ajili ya kuuza kwa wateja wake katika Soko Kuu la Kariakoo.

Ukaguzi huo ulifanywa na maofisa wa FCC, Jeshi la Polisi na Mmiliki wa Kampuni ya Rungu ambayo inadai bidhaa zake zimekuwa zikitolewa nakala na kampuni nyingine.

"Siwezi kujibu vyema Kiswahili, nitaongea lugha yangu ya Kisukuma, hizi bidhaa 'nyembe' ninanunua kutoka kwa machinga, aliniletea maboksi 10, moja ninanunua kwa Sh. 300,000," alidai Njira katika tafsiri iliyo rasmi ya kile alichokiwasilisha kwa lugha ya Kisukuma.

Meneja Mauzo wa Kampuni ya Rungu, Noel Lema, alisema mbali na kutengeneza bidhaa zao halisi, wapo wafanyabiashara wasio waaminifu ambao wanatoa bidhaa zinazofanana na zao.

"Hawa ni watu wanaingilia biashara yetu kwa kutengeneza bidhaa kama zetu na kuziuza kwa bei nafuu na sisi kukosa soko la biashara," alilalamika.

Alifafanua kuwa bidhaa walizokamata za nyembe wametengeneza nembo za Rungu lakini zenyewe hazina ubora, zinavunjika haraka, lakini ubora wake haujathibitishwa, hivyo zinaweza kusababisha madhara kwa watumiaji.

Alisema boksi moja la nyembe wanazouza ni Sh. 590,000 lakini feki zimekuwa zikiuzwa kati ya Sh. 300,000 na 400,000.

"Tunatoa wito kwa serikali itusaidie kushirikiana na sisi kukomesha vitendo hivi hasa kwa kuzingatia kuwa tunalipa kodi, lakini wasiolipa kodi ndio wanaozalisha bidhaa feki na kusababisha kudorora kwa bidhaa zetu," anasema.

Lyimo alisema kuwa mbali na mfanyabiashara huyo, walikamata bidhaa nyingine tani tatu za nyembe maarufu kama Rungu Max.

Maofisa wa FCC baada ya kufanya ukaguzi, walisema hawawezi kutoa taarifa yoyote kwa vyombo vya habari hadi hapo watakapotoa taarifa rasmi kwa vyombo vya habari kuhusu operesheni hizo ambazo hufanywa mara kwa mara.

Maofisa wa polisi walioshiriki operesheni hiyo waliondoka na mfanyabiashara huyo pamoja na bidhaa alizokamatwa nazo.

## HABARI KITAIFA

# Sabaya adaiwa kuchukua mamilioni kwa m/biashara

**Na Allan Isack,** ARUSHA

ALIYEKUWA Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya na wenzake, jana walisomewa maelezo ya awali katika kesi inayowakabili ya uhujumu uchumi.

Washtakiwa wengine ni Silvester Nyengu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).

Akiwasomea maelezo ya awali ya mashtaka yanayowakabili washtakiwa hao katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Filex Kwetukia, alidai washtakiwa wanakabiliwa na shtaka la kwanza la kuongoza genge na shtaka la tano la utakatishaji wa fedha.

Alidai kwamba shtaka la pili ni la kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Shtaka la tatu ni la kujihusisha na vitendo vya rushwa, shtaka la nne linahusu matumizi mabaya ya madaraka yanayomkabili Sabaya peke yake.

Wakili huyo wa serikali alidai kwamba Januari 22, mwaka huu, washtakiwa hao wakiongozwa na Sabaya, walikwenda katika gereji inayomilikiwa na Francis Mroso eneo la Mbauda jijini Arusha na walipofika katika gereji hiyo, walimtuhumu mmiliki kwamba ni mkwepaji wa kodi na alikuwa akifanya biashara bila ya kutoa risiti za kielektroniki Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Ilidaiwa zaidi kwamba Sabaya na wenzake walimtuhumu Mroso, kwamba alikuwa akitoa vipuri vya magari kutoka nje na kuingiza nchini bila ya kufuata utaratibu wa kisheria. "Baada ya kumpatia tuhuma hizo, Sabaya alimtishia Mroso kuwa asipofuata maelekezo yake watamfungulia kesi ya uhujumu uchumi na utakatishaji wa fedha.

"Kutokana na vitisho hivyo, Mroso, alimuuliza Sabaya kwamba afanye nini ili wasimfungulie mashtaka hayo na mshtakiwa huyo alimweleza kuwa atoe Sh. milioni 90 ili awe huru," alidai.

Kadhalika Wakili huyo wa Serikali, alidai Sabaya, walinzi wake na Mroso waliambatana hadi Benki ya CRDB Tawi la kwa Murombo, kwenda kutoa fedha hizo kwenye akaunti kwa ajili ya kumpatia.

"Mroso alikubali kuwapa fedha hizo, akiwa katika mazingira ya kulazimisha kwa kuwa alikuwa chini ya usimamizi wa walinzi wa

Sabaya na baada ya kutoa fedha hizo kwenye akaunti walikwenda naye hadi eneo la Sombetini jijini Arusha ndio alipokabidhi fedha hizo," alidai Wakili huyo.

Aidha, alidai baada ya Sabaya kupokea fedha hizo, walimruhusu kuondoka eneo hilo, huku wakimsisitiza kwamba watarejea kwenda kuangalia kama anafanyabiashara na kutoa risiti za TRA na kama anafuata utaratibu wa kuingiza bidhaa kutoka nje ya nchi.

Vile vile, alidai kwamba Sabaya akiwa mtumishi wa serikali kwa nafasi ya Mkuu wa Wilaya ya Hai, alitumia vibaya madaraka yake kwa kuwa alipaswa kuwa kwenye kituo chake cha kazi na hakupaswa kutoka bila kupewa ruhusa na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro.

"Hakuzingatia miongozo na kanuni za utendaji kazi wake, kwa kuwa alitoka kwenye kituo cha kazi bila ya kufuata utaratibu wa kisheria na alitumia magari kwenda Arusha na kujifanya ofisa wa kodi, kitu ambacho ni kinyume cha sheria.

"Upelelezi wa shauri hili unaonyesha kwamba baada ya kupata fedha hizo, walijigawia na hii inaonyesha kwamba mtuhumiwa wa kwanza (Sabaya) alikiuka kanuni za utendaji kazi akiwa kama Mkuu wa Wilaya kwa kuwa alilazimisha kupata fedha kwa kutumia nguvu," alidai Kwetukia.

Baada ya washtakiwa hao, kusomewa maelezo ya awali, Hakimu wa Mahakama hiyo, Patricia Kisinda, aliahirisha shauri hilo hadi Septemba 23 na 24 mwaka huu, kesi hiyo itakapotajwa tena.

Upande wa Jamhuri ulisema utakuwa na mashahidi 20 na vielelezo 16.

# CCM yaitaka Wizara ya Nishati kumaliza kero kukatika umeme

**Na Beatrice Shayo,** NACHINGWEA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimeiagiza Wizara ya Nishati kuhakikisha inatafuta suluhu ya kukatika kwa umeme kila wakati nchini ikiwamo katika Wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Shaka Hamdu Shaka, alitoa agizo hilo juzi wakati akizungumza na wananchi wa shina namba moja la Nambambo na shina namba mbili la Namatula ambao walimlalamikia kuwapo kwa tatizo la kukatika kwa umeme kila wakati na hata vifaa vyao kuungua pamoja na ubovu wa barabara.

Shaka alisema hawataweza kuvumilia changamoto za kuwaumiza wananchi na ndiyo maana wameamua kufanya ziara katika mashina ili kuwakumbusha viongozi wajibu wao katika kutatua kero za wananchi.

"Hatutamvumilia mtumishi yeyote ambaye amepewa dhamana na serikali yetu halafu yeye akafanya vile ambavyo anataka yeye, chama hakitamvulimia na ndiyo maana tumekuja kuwasikiliza na kuwauliza viongozi wana mipango gani," alisema Shaka.

"Nimepewa taarifa hapa kuna mama kajinyima kanunua jokofu lake sasa hivi limekufa kwa umeme kukatika mara kwa mara, hapa tunawasaidia wananchi ama tunawarudisha nyuma."

Katika kushughulikia tatizo hilo, Shaka alimpigia simu Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato na kuiweka sauti yake wazi kwa wananchi (loud speaker) ili wamsikie na kumuuliza ni lini atatatua tatizo hilo la kukatika umeme kila wakati katika wilaya hiyo.

Byabato alisema wanaendelea kusimamia na kutekeleza yale ambayo wameyaahidi kwenye Ilani ya CCM.

Alisema walikuwa na kikao cha kufuatilia kwa nini siku za hivi karibuni kumekuwa na changamoto ya kukatika kwa umeme mara kwa mara.

NMB
Karibu yako

KUTOA HUDUMA BORA ZA KIBENKI
KWA WOTE NI JADI YETU

Tuzo ya International Banker - Ubunifu wa Huduma za Wateja Binafsi Tanzania 2021

Tuzo ya International Business Magazine - Benki Bora Wateja Binafsi Tanzania 2021

Tuzo za World Economic Banking - Benki Bora ya Biashara na Benki Bora ya Huduma za Uwekezaji Tanzania 2021

Asante kwa Kuchagua NMB Bank!




www.nmbbank.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Maji yatumike vizuri

**JUZI** Bonde la Wami/Ruvu lilisitisha kutoa vibali vipya vya uvunaji maji katika bonde hilo pamoja na kuwataka wananchi kuacha mara moja kufanya shughuli za kibinadamu kwenye nyanzo vya mito.

Lilieleza kuwa hatua hiyo imechukuliwa baada ya kupungua kwa kina cha maji katika chanzo hicho kutokana na upungufu wa mvua kwa msimu huu na ujao pamoja na kuongezeka kwa shughuli za kibindamu.

Sababu kubwa ni kupungua kwa kina cha maji ikilinganishwa na Septemba mwaka jana, kilipokuwa na kina cha milimita 12,500 hadi kufikia 7,500 kwa sasa.

Kwa mujibu wa Bonde hilo, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) inachukua milimita 5,000 kwa sekunde kutoka katika mto huo. Aidha, walitahadharisha kuwa kama hali ya ukame itaendelea, mto huo utakauka na kusababisha mitambo ya DAWASA kupungua uwezo wa uzalishaji maji na kuhudumia wakazi wa Dar es Salaam na Pwani.

Jitihada za awali ni kuweka sandarusi (maarufu kama viroba) kuongoza maji kwenda kwenye mitambo yao ili kukabiliana na upungufu huo. Tunafahamu kuwa mabadiliko ya tabianchi ni mojawapo ya chanzo cha uhaba wa maji duniani, uwapo wa ukame na ongezeko la joto kuna changia kwa asilimia kubwa kukauka kwa mabwawa na vyanzo vya maji.

Mabadiliko ya tabianchi yanaathiri kiasi cha maji yanayohitajika kwa matumizi na kwa hivyo kuathiri haki ya msingi ya binadamu kwa mabilioni ya watu ya kutumia majisafi na salama kwa matumizi mbalimbali.

Hivyo, mamlaka husika zinapaswa kuhakikisha zinadhibiti hali ya uharibifu wa mazingira miongoni mwa wakulima wanaolima pembezoni mwa kingo za maji, wanapaswa kuondolewa kwa mujibu wa sheria ya mazingira inayopiga marufuku kutofanyika kwa shughuli zozote ndani ya mita 60 kutoka kwenye vyanzo vya maji.

Mbali na hilo, jamii inapaswa kuelimishwa kuhusu matumizi makubwa ya maji hususani ya kuogea, kufulia, kupikia, tabia ya watu kutumia maji kwa fujo inapaswa kupunguzwa.

Tukumbuke kuwa utunzaji wa vyanzo vya maji ni jukumu la watu wote, kwani kuacha vyanzo hivyo vikatumika kiholela au kuharibiwa, madhara yake ni makubwa kwa kila binadamu.

Suala la kufanya shughuli za kibinadamu kando ya vyanzo vya maji kama vile ulimaji kunasababisha ubora wa maji kupungua kwani mbolea inayotumika katika kilimo huenda ardhini na kuingia katika tabaka la maji na kuaribu ubora wa maji.

Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) mwanzoni mwa mwezi huu ilitoa taarifa ya tahadhari ya hapo baadaye kuwapo kwa ukame katika baadhi ya mikoa inayopata mvua mara mbili kwa mwaka, hali ambayo iliyowahi kutokea miaka 16 iliyopita. Kutokana na tahadhari hiyo, mamlaka husika kwa maana ya serikali inapaswa kutoa elimu ya matumizi sahihi ya maji kwa wananchi.

Wananchi wanapaswa kuwa na matumizi mazuri ya maji hususani majumbani ambako kunaelezwa baadhi ya jamii zimekuwa na matumizi mabaya. Tabia ya watu kuoga mara tano, kufua kila siku ama kuosha vyombo kwa kutumia ndoo ya ujazo wa lita20 kunapaswa kupunguzwa, kubana matumizi kunapaswa kuzingatiwa.

Kadhalika, wakulima wakubwa wenye mashamba yenye hekari 10 na kuendelea wanapaswa kuanza kuchukua hatua ya kubana matumizi ya maji. Kama mkulima alikuwa amefunga mfumo wa umwagiliaji siku nzima anapaswa kupanga muda maalum wa umwagiliaji. Ni jukumu la kila Mtanzania kuhakikisha anatunza vyanzo vya maji, kutokufanya hivyo kutasababisha sehemu ya jamii hususani wanawake na watoto kulazimika kutembea umbali mrefu kutafuta maji.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com







Na Beatrice Inyasi, TURDACO

## Muungwana Lazima Nilonge

# Utitiri wa vibanda vya biashara Dar, kero tupu

**KWA** tathmini ya kawaida, nadiriki kutamka ni jiji la wajasiriamali. Ndivyo ilivyo katika jamii za maeneo mengi kitaifa na hasa mijini, kwani vijijini kwa kiasi kikubwa wakulima wameshika hatamu

Ni kupitia uzoefu huo, kuna vibanda vya wafanyabiashara wadogo wengi jijini Dar es Salaam na kadri mji inavyokuwa kwa ongezeko la wakazi, ndivyo inavyojikisi kwa wanaosaka shughuli za kujiendeza kimaisha.

Hapo ina maana kwamba watu wanakurupuka kusaka shughuli za kufanya. Ni kweli kwamba hilo ni jambo la haki na wajibu kwa kila mtu aliye na umri zaidi ya miaka 18, atatafute riziki kwa ajili ya kutimiza mahitaji yake.

Busara, ni kwamba riziki hiyo itafutwe kwa njia ambayo haitambugudhi mwingine, wala haitaingilia mipaka ya wengine hao kimaisha. Niseme, hapo ndipo penye shida!

Ukweli ni kwamba kwa tunayoyaona Dar es Salaam, wafanyabiashara hao wamekuwa mithili ya kero kwa baadhi ya watu na umma kwa jumla. Kuingiliana mtindo mmoja.

Mtu hata unapothubutu kupiga hatua jijini humu kwa azma yoyote ile, lazima katika kona zake tofauti unazokatisha wamejaa wajasiriamali na nielekeze mfano wafanyabiashara hasa maeneo ya katikati ya mji.

Naenda mahsusi, eneo ililo Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), mpaka kufikia iliko Maktaba Kuu ya Taifa, hakuna atakayepinga kuwa eneo hilo limepoteza mwonekano wake wa asili.

Vibanda vya biashara vimekuwa vingi, katika hali inayoleta shida kubwa hata kwa wapita njia, mana ni eneo walikotengewa wapita njia.

Sio eneo hilo pekee, yapo maeneno mengi kama mtu umepita wastani wa miezi mitatu sasa hujafika na hasa katikati maeneo ya jiji au palikochangamka kibiashara, unaweza kubaki katika mashangao.

Jiji limepoteza mwonekano wake, kutokana na msongamano wa vibanda hivyo vya biashara, ingawa serikali inajitahidi sana kutengeneza miundombinu itakayofanya jiji lizidi kuvutia.

> **Jiji limepoteza mwonekano wake, kutokana na msongamano wa vibanda hivyo vya biashara, ingawa serikali inajitahidi sana kutengeneza miundombinu itakayofanya jiji lizidi kuvutia.**

Inawezekana ruhusa waliyopewa ndugu zetu hao katika fursa hizo za kutafuta maisha, hasa kupitia haki ya kuwa na kitambulisho cha wajasiriamali ndiyo imetufikisha hapa leo. Kweli kizuri hakikosi kasoro!

Najiuliza, mbona serikali ilikuwa na nia njema sana kwa wananchi wake, kuhakikisha kila mtu anyeweza kujiajiri na afanye hivyo, huku nao wakijiingizia kipato kwa nembo la vitambulisho hivyo.

Ni vizuri watu wakafanya biashara zao bila ya kusumbuliwa na mamlaka zozote, lakini sura ya pili wahakikishe mazingira yao yanakuwa rafiki.

Kwa bahati mbaya sasa, ikitokea ajali ya moto watu wengi watadhurika kutokana na mpangilio mbovu wa maeneo hayo.

Watu wanaweza kufanya biashara na bado jiji likawa katika hali inayopendeza kimazingira usafi na mpangilio wake, kila mtu akabaki anafurahia hali.

Ni miezi michache iliyopita, Mkuu wa Wilaya ya Morogoro Mjini, Albert Msando, alionyesha mpango wa kuwasaidia wafanyabiashara wadogo wilayani humo. Ni jambo jema sana.

Akishirikiana na baadhi ya wadau, wametengeneza vibanda vya namna fulani vizuri ambavyo vinafanana kwenye mstari mmoja na vinapendeza mpaka basi!

Ni mradi ambao ukikamilika, utawasaidia wafanyabiashara kukaa katika mazingira yanayopendeza, pia mazingira nayo yataonekana sio mazuri.

Msisitizo wangu ni katika imani serikali ina nia njema kwa wafanyabiashara na wala wasizuiliwe kufanya yao. Mamlaka za kiserikali katika maeneo husika nazo zina wajibu kuangalia namna zitakavyohakikisha jiji linakuwa katika mandhari inayopendeza na watu wanaingiza vipato.

HABARI KITAIFA

## CAG Zanzibar kuanza na udhibiti mapato

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Zanzibar, Dk. Othman Abass, amesema ataishauri serikali juu ya ukusanyaji wa mapato ikiwamo kudhibiti mianya inayosababisha kupotea au kuvuja.

Dk. Othman alisema hayo baada ya kuapishwa kushika wadhifa huo mbele ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi. Aliteuliwa hivi karibuni na maofisda wengine kushika nafasi mbalimbali katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ).

Alisema mapato ya serikali yamekuwa yakipotea kutokana na sababu mbalimbali, hivyo ataishauri serikali namna ya kuyadhibiti na njia sahihi za kuchukua katika kuongeza mapato.

Akizungumzia ripoti aliyoiwasilisha kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Mwinyi miezi mitatu iliyopita, alisema tayari inafanyiwa kazi.

Dk. Juma Yakuti Juma, Naibu Katibu wa Baraza la Mapinduzi alisema nafasi aliyopewa ina majukumu makubwa ndani ya serikali hivyo aliahidi kuitumikia kwa nguvu zote na uadilifu mkubwa kwa kushirikiana na watendaji wengine.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Micheweni Pemba, Mgeni Khatib Yahya, ambaye alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Wete, alisema uteuzi huo ameupokea kwa furaha kubwa na kuahidi kufanya kazi kama walivyoelekezwa na Rais Mwinyi katika kuwatumikia wananchi.

Alisema kubadilishwa mkoa mwingine na kiongozi mkuu wa nchi inatokana na utendaji mzuri wa kazi zake katika kuwatumikia wananchi.

Akizungumzia changamoto zilizokuwapo katika wilaya hiyo ikiwamo wanafunzi kutokwenda shuleni, alisema atahakikisha analisimamia kila mtoto apate haki yake ya elimu.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini 'B' Unguja, Hamid Seif Said, aliahidi kufanya kazi hasa katika kushughulikia migogoro ya ardhi.

Katika kutekeleza hilo, aliahidi kushirikiana na masheha katika kufanyia kazi migogoro hiyo na kuwaomba wananchi kumpa ushirikiano.

RAIS Mwinyi jana aliwaapisha viongozi mbalimbali aliowateuwa hivi karibuni katika taasisi za serikali akiwamo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hafla ya kuapishwa viongozi hao ilifanyika Ikulu Zanzibar. Wengine walioapishwa ni Khatib Juma Mjaja kuwa Mkuu wa Wilaya ya Mkoani Pemba na Hamad Omar Bakar kuwa Mkuu wa wilaya ya Wete Pemba na Kubingwa Mashaka Simba kuwa Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma.

# TPFS yaridhishwa mikakati ya serikali kukuza biashara

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) imekiri uwapo wa ongezeko la biashara kati ya Tanzania na nchi za Ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na ushoroba wa kusini zikiwamo nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) tangu Rais Samia Suluhu Hassan aingie madarakani.

Mwenyekiti wa TPSF, Angelina Ngalua, alisema jana mkoani Dar es Salaam kuwa ukuaji wa biashara kati ya Tanzania na nchi jirani, zikiwamo Kenya, Burundi na Uganda, umeongezeka huku ushirikiano kati ya Tanzania na mataifa hayo ukiimarika kuashiria kukua kwa diplomasia ya uchumi. "Sasa hivi ukiangali ukuaji wa biashara chini ya uongozi wa serikali ya awamu ya sita, serikali inaishirikisha ipasavyo sekta binafsi katika kukuza na kuendeleza biashara na uwekezaji nchini," alisema.

Aliongeza kuwa ushirikiano ambao serikali imekuwa ikiutoa kwa sekta binafsi umechangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa kiwango cha biashara kati ya Tanzania na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na ushoroba wa kusini ikihusisha nchi za SADC. Kiongozi huyo wa TPSF alipongeza hatua ya Rais Samia Suluhu Hassan kuamua kuambatana na wawekezaji na wafanyabiashara kutoka katika taasisi hiyo, akisisitiza kuwa hatua hiyo imesaidia kuwakutanisha na kuwaunganisha na wenzao wa mataifa mengine tofauti na nyakati zilizopita ambapo kila mfanyabiashara alijitafutia fursa mwenyewe.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, aliihakikishia TPSF ushirikiano mkubwa kutoka serikalini kwa kuwa serikali inaamini uwapo wa sekta binafsi imara ni kichocheo kikubwa cha ukuaji wa uchumi imara wa nchi.

Balozi Mulamula aliitaka TPSF kuhakikisha inakuwa na kanzidata ili kurahisisha azma ya serikali ya kuiunganisha sekta hiyo na wafanyabiashara pamoja na wawekezaji kutoka katika mataifa mengine ulimwenguni.

Katika tukio lingine, waziri huyo amekutana kwa mazungumzo na Mkurugenzi anayeshughulikia masuala ya maendeleo ya uchumi, Dk. Stefan Oswald, aliyefuatana na mkurugenzi anayeshughulikia masuala ya Afrika katika Wizara ya Mambo ya Nje wa Ujerumani kwa lengo la kuzungumzia masuala mbalimbali ikiwamo ushirikiano wa kidiplomasia na maendeleo ya Uchumi.

Dk. Oswald alibainisha kuguswa na ishara ya mabadiliko ya kidiplomasia na ushirikiano wa maendeleo na mataifa mengine duniani iliyoonyeshwa na Rais Samia. Aliongeza kuwa mazungumzo kati ya Rais Samia na Kansela wa Ujerumani, Angela Merkel, ambayo yalilenga kutoa kipaumbele cha uwapo wa mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji, yamekuwa kichocheo cha viongozi hao kufanya ziara nchini.

Dk. Stefan alisema Ujerumani iko tayari kushirikiana na Tanzania pamoja na nchi zingine za Afrika kuzisaidia kuimarisha uchumi kutokana na kuathiriwa na UVIKO-19.






# Serikali yazindua mpango wa chanjo tembezi nchini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imezindua mpango wa jamii shirikishi na harakishi wa chanjo dhidi ya UVIKO-19 wenye mambo 10 ikiwamo kuwapo kwa chanjo tembezi (mobile vaccination site) na kuwafuata wananchi walio tayari kuchanjwa kwa hiari.

Mpango huo ulizinduliwa jana na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, Dk. Dorothy Gwajima, kwenye mkutano mkuu wa mwaka wa waganga wakuu wa mikoa na halmashauri uliofanyika jijini hapa. Akitoa maelezo ya mpango huo, Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi, alisema mpango huo unalenga kuongeza vituo vya kuchanja kutoka 550 hadi 6,784, kuharakisha wananchi kuchanjwa mapema.

"Kwenye chanjo tembezi magari tumeshaagiza na nimeagiza tangu juzi, taasisi zetu na halmashauri zitoe magari kwa ajili ya kutekeleza huu mpango, nimesikia baadhi ya wakurugenzi wanasuasua kutoa magari, MSD na Mpango wa chanjo wametoa, TB bado hawajatoa, huu ni mpango wa kitaifa, nataka yatoke ndani ya saa 24 zijazo kwa taasisi zote ambazo bado," alisema.

Alisema utasimamiwa na wakuu wa mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa na Waganga Wakuu wa Mikoa.

"Ni mwezi sasa tangu Rais Samia Suluhu Hassan azindue utoaji chanjo ambapo watu zaidi ya 350,000 hadi sasa wamechanja, bado tunahitaji wananchi wachanje mapema iwezekanavyo kutokana na asili ya ugonjwa wenyewe," alisema. Alisema ugonjwa huo ni wa mlipuko na unasambaa haraka na uchanjaji ni njia pekee ya kupunguza maambukizi ya ugonjwa huo.

Alibainisha kuwa vikundi, viongozi wa kijamii na serikali za mitaa ndiyo muhimili wa kuhamasisha chanjo mijini na vijijini.

"Mpango huo pia unalenga elimu itatolewa kupitia njia za asili za ngoma, kwaya, muziki, maigizo, semina, mikutano na pia TV na redio jamii, kutumia pia viongozo wa serikali, kijamii, kidini, wabunge, wasanii, watu maarufu, wataalamu, wawakilishi wa vikundi vya kijamii kama vile Vicoba," alisema. Alisema kila halmashauri itakuwa na lengo la kufikia kwa muda maalum utakaopangwa na kuwafuata wananchi walio tayari kuchanjwa bila wao kulazimika kwenda vituoni.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe, alisema lengo la mpango huo ni kuharakisha utoaji chanjo kwa kuwa hadi sasa haujafikia nusu ya chanjo zilizoletwa zaidi ya milioni moja.

"Tutakutana na wakuu wa mikoa na timu mbalimbali kama sehemu ya uraghabishi na kupata nafasi ya kutoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali, RMO utahitajika kufanya hili, tutatumia redio za kijamii," alisema.

Aliwataka waganga hao kufuatilia matumizi ya fedha za mpango huo na kutoa taarifa ya matumizi yake kwake na fedha zitapelekwa wiki ijayo kwa Wakurugenzi wa Halmashauri kwa ajili ya kazi hiyo.



Baadhi ya watoto wa miaka minne hadi 15 wa Kanisa la Waadventista Wasabato Jimbo la Kusini Mashariki Tanzania, wakiwa katika mafunzo ya kuwanoa kiakili, kimwili, kiroho na kijamii yaliyoandaliwa na Idara ya Huduma za Vijana ya kanisa hilo na kufanyika kwa siku tatu eneo la Kwembe, mkoani Dar es Salaam. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Waziri ataka usimamizi wa mpango kabambe Geita

**Na Munir Shemweta,** GEITA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amezindua Mpango Kabambe wa Mji wa Geita (2017-2037) na kuitaka Halmashauri ya Mji kusimamia utekelezaji wake bila kuruka hatua za utekelezaji.

Uzinduzi wa mpango huo ulifanyika juzi mjini hapa na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwamo madiwani, wawakilishi wa taasisi za serikali, watumishi wa sekta ya ardhi, viongozi wa dini na wananchi. Alisema Mkoa wa Geita umebahatika kuwa na shughuli nyingi zikiwamo za uchimbaji dhahabu na kuufanya kupewa jina la 'mji wa dhahabu'. Alisisitiza kuwa fursa ya dhahabu ikitumika vizuri, italeta mapinduzi ya haraka ya kiuchumi na kijamii. Naibu Waziri alisema Geita ina wachimbaji wengi wa madini na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na Wizara ya Madini, inaangalia namna bora ya kuwatambua wachimbaji wadogo wote, ili wapate fursa ya kumiliki maeneo yao kwa kuwa na hati ya umiliki wa ardhi. "Wachimbaji wadogo wana leseni za uchimbaji madini, lakini mgogoro huku juu ni mkubwa sana kwa sababu tu hawajatambulika," alisema.

Dk. Mabula aliongeza kuwa hata namna ya kuwawezesha wachimbaji hao wadogo kupitia ardhi kutawawezesha kufanya kazi kwenye madini huku pia wakipata mkopo benki kupitia hati za umiliki ardhi, hivyo kuwawezesha kufanya kazi zao vizuri.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, mpango kabambe uliozinduliwa katika utekelezaji wake utakwenda sambamba na kuwawezesha wachimbaji wadogo kuwa na uhakika na usalama wa miliki zao katika maeneo wanayofanyia kazi.

Mbunge wa Geita Mjini, Constatine Kanyasu, alisema mpango kabambe huo unatoa dira ya mji kuelekea kwenye manispaa kwa kuwa haiwezekani kuwa na manispaa isiyo na mpango. Alisisitiza kuwa yeye na wananchi wake wamefarijika kwa kuzinduliwa mpango huo kabambe wa mji wa Geita.

Naye Mkurugenzi Msaidizi wa Maendeleo ya Makazi katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Imaculate Senje, aliiomba Halmashauri ya Mji wa Geita wakati wa utekelezaji wake ihifadhi maeneo yote yaliyoainishwa katika mpango kulingana na mahitaji na kutolea mfano kama eneo limetengwa kwa ajili ya viwanda basi lihifadhiwe kwa shughuli hiyo.

Halmashauri ya Mji wa Geita ilianzishwa na kutangazwa rasmi mwaka 2002 na ndiyo makao makuu ya mkoa wa Geita na ni kitovu cha shughuli nyingi za kiutawala, kijamii na kiuchumi kwa mkoa hali inayosababisha ukuaji wa haraka wa idadi ya watu na shughuli za kiuchumi katika mji huo.

# NMB yashinda tuzo kimataifa

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB, kwa mwaka huu imeshinda tuzo nne za kimataifa, zote zikiitaja kuwa Benki bora zaidi Tanzania.

Tuzo hizi zinafanya jumla ya tuzo zote ambazo NMB imezipata mwaka 2021, kufikia sita.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna, alisema kupata tuzo hizo kunatokana na NMB ni benki kuwa rafiki kwa wateja wake.

Tuzo hizo ni pamoja na Tuzo ya Benki Bora ya Biashara na Benki Bora ya Huduma za Uwekezaji Tanzania mwaka 2021, zote kutoka Jarida la World Economic Banking, tuzo ya Benki Bora kwa Ubunifu wa Huduma za Wateja Binafsi kutoka Jarida la International Banker na tuzo ya Benki Bora ya Wateja Binafsi kutoka Jarida la International Business.

"Tuzo hizi zinaendana na dira yetu ya kuifanya NMB kuwa benki bora zaidi Tanzania, sote tufahamu kuwa tuzo hizi ni za kimataifa zimetolewa na majarida yanayoaminiwa na taasisi za kifedha duniani, hivyo zimezingatia vigezo, ufanisi na utendaji wetu," alisema Zaipuna.

Mapema mwaka huu, Benki ya NMB ilitajwa kwa mara ya tisa mfululizo kuwa Benki bora zaidi Tanzania na Jarida la kimataifa la Euromoney na Benki bora ya wateja Binafsi kutoka Jarida la Global Banking and Finance. Hizi ni tuzo za juu kabisa za ubora zinazotolewa na majarida makubwa duniani yenye makao yake makuu jijini London na nchini Marekani.

Zaipuna alisema tuzo hizo zimetolewa kwa kuzingatia vigezo kadhaa kwa benki vilivyopendekezwa vya ufanisi wa mahesabu na utendaji kwa ujumla, mkakati wa huduma za kidijitali, huduma jumuishi za fedha, usalama wa huduma za kimtandao na uwajibikaji wa benki katika jamii inayoizunguka.

"Leo hii, zaidi ya asilimia 93 ya miamala yote ya benki ya NMB inafanyika nje ya matawi ya benki. Vigezo vingine vilivyotumika ni mtaji wa benki, mapato yatokanayo na mali za kampuni, uwiano wa fedha na gharama za uendeshaji, kiwango cha amana za wateja, kiwango cha mkopo katika soko, uwiano kati ya mikopo na amana za wateja, uwiano wa mikopo isiyolipika, na uwiano wa hasara itokanayo na mikopo isiyolipika," alisema.

"Tuzo hizi zinadhihirisha nafasi ya uongozi wa Benki ya NMB katika sekta ya kibenki nchini. Jopo la majaji wa tuzo zote nne waliona kuwa huduma za kidigitali na za uwakala pamoja na mchango wa benki katika jamii, zimechangia katika ushindi huo," alisema Zaipua na kuongeza:

"Tunaendelea kuwekeza katika tekinolojia na mtandao wetu wa matawi kwa makini sana na kuongeza nguvu kwenye ubunifu ili kuendelea kutoa suluhishi bora za huduma sokoni."

Kwa miezi 12 iliyopita, Zaipuna alisema benki imeendelea kuboresha huduma zake ili kufikia mahitaji ya wateja, hivyo kuziba pengo la huduma na suluhishi za kifedha sokoni.

Kwa mujibu wa Zaipuna, uwekezaji wa teknolojia umechangia kupanua wigo wa mtandao wake na kurahisisha ukamilishaji wa miamala hivyo kuboresha zaidi huduma kwa wateja.

# Vodacom Foundation yaipiga jeki hospitali

**Na Mwandishi Wetu,** MASASI

HOSPITALI ya Mkomaindo wilayani Masasi, mkoani Mtwara, itaondokana au kupunguza vifo vya watoto wachanga vitokanavyo na changamoto mbalimbali, baada ya kukabidhiwa msaada wa vifaa tiba kutoka Taasisi ya Vodacom Tanzania Foundation.

Pia, watoto njiti katika hospitali hiyo wataondokana na changamoto ya kukaa wawili katika mashine maalumu (incubator), baada ya kusaidiwa nyingine na taasisi hiyo.

Wakikabidhiwa vifaa hivyo vyenye thamani ya Sh. milioni 67, jana, Kaimu Mganga Mkuu Halmashauri ya Mji Masasi, Dk. Amina Moshi, alisema vifaa tiba hivyo vimelenga kitengo cha uzazi kwa mama na watoto wachanga, hivyo vitasaidia kuboresha huduma za afya.

"Tulikuwa na changamoto ya vifaa tiba vinavyoweza kusaidia watoto wachanga kupata joto baada ya kuzaliwa na incubator kwa ajili ya watoto njiti waliozaliwa kabla ya kutimiza miezi tisa... vifaa vingine kama mashine za oksijeni vitawasaidia katika kupumua kwa wale wenye tatizo la kupumua baada ya kuzaliwa," alisema Dk. Amina.

Alibainisha halmashauri hiyo imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya vifo vya watoto wachanga ambapo Januari hadi Desemba 2020 kulikuwa na vifo vya watoto wachanga 165 na Januari hadi Julai 2021 kumekuwa na vifo 63.

Alisema kwa upande wa vifo vya kinamama Januari hadi Desemba 2020 vifo vitokanavyo na uzazi vilikuwa 10 na Januari hadi Julai 2021 vilikuwa vifo sita hivyo msaada huo wa vifaa tiba vitasaidia sana kupunguza vifo hivyo.

Mkurugenzi wa Vodacom Tanzania Foundation, Rosalynn Mworia, alisema taasisi hiyo imekuwa ikishirikiana na serikali katika maeneo mbalimbali kama afya na kilimo ili kugusa jamii hususani katika afya ya uzazi.

Alisema wamekuwa wakifanya uhamasishaji na kampeni mbalimbali kwa kutumia mtandao wa simu kwa kutuma ujumbe mfupi pamoja na njia nyingine za mawasiliano ili kupeleka taarifa mbalimbali za afya kama tatizo la fistula.



Waziri wa Uwekezaji, Geoffrey Mwambe (kushoto) na Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Claudia Kitta (kulia), wakipokea baadhi ya vifaa tiba kutoka kwa Mkurugenzi wa Vodacom Tanzania Foundation, Rosalynn Mworia, kwa ajili ya kusaidia utoaji huduma za matibabu kwa watoto njiti katika Hospitali ya Mkomaindo, wilayani humo, mkoani Mtwara juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi kaya maskini kupata mikopo kwa 100%

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BODI ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HELSB) na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), zimeingia makubaliano ya kutoa mkopo wa asilimia 100 kwa wanafunzi wanaotoka kaya maskini nchini.

Aidha, bodi imetenga Sh. bilioni 570, kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi 160,000 kwa mwaka wa fedha ujao wa masomo 2021/22.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa kusaini makubaliano hayo Katibu Mkuu Ikulu ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya TASAF, Moses Kusiluka, alisema serikali ina dhamira kubwa ya kuhakikisha wanafunzi wote wanapata mikopo kwa asilimia zote ili kutimiza ndoto zao. Alisema lengo lao ni kuona mikopo inapatikana kwa walengwa halisi ili kuondoa mkanganyiko watu kupata mikopo ambao hawatoki katika kaya maskini.

"Serikali inahakikisha dhamira ya Watanzania wahitaji wenye sifa za kujiunga na elimu ya juu wanapata mikopo na kupata elimu ya juu," alisema Kusiluka.

Alifafanua kuwa jambo lililowakutanisha hapo ni pamoja na kuhakikisha makubaliano hayo yanafanyika kikamilifu ili wanafunzi walengwa wapate mikopo kwa asilimia zote.

Mwakilishi wa Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambaye ni Mkurugenzi Msaidizi wa Rasilimali Watu, Sebastian Inoshi, alisema serikali ina dhamira ya kuhakikisha wahitaji wenye sifa za kujiunga na elimu ya juu wanapata mikopo.

Alisisitiza kuwa ni muhimu kwa taasisi za serikali kushirikiana katika kuhakikisha wanawafikia wananchi na kutoa huduma.

"Ni muhimu TASAF na Bodi ya Mikopo kuhakikisha makubaliano hayo yanatekelezwa kikamilifu kama inavyotarajiwa," alisema.

Hata hivyo, aliiagiza TASAF na Bodi ya Mikopo kuhakikisha inaandaa taarifa ya utekelezaji wa makubaliano haya na kuyawasilisha wizarani na bodi iendelee kubaini wadau muhimu wa kimkakati.

Alisema pia taasisi hizo zinapaswa kuongeza kasi ya kuunganishwa katika mfumo wa TEHAMA, ili kuwezesha utambuzi wa haraka na uhakika kwa wanafunzi wanaotoka katika kaya maskini.

Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Ladislaus Mwamanga, alisema kusainiwa kwa makubaliano hayo kunafungua ukurasa mpya ambapo sasa watoto wa maskini wanakwenda kusoma bila kikwazo.

Mwamanga alisema wengi wa waombaji kuanzia mwakani hawatakuwa na usumbufu kwenye maombi yao, kwa kuwa watatambuliwa na mfumo, ambao utakuwa mmoja kwa taasisi zote mbili.

Kuhusu gharama za masomo kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi sita, alisema fedha zinazotolewa ni msaada na ruzuku, hivyo kwao haijawa mikopo, jambo linalofanya wasidaiwe wanapomaliza elimu ya kidato cha sita.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo, Abdul Razaq Badru, alisema safari hii fedha za mkopo zimeongezwa, hivyo wanafunzi watakaochaguliwa watapata mkopo stahiki.

Alisema lengo ni kuona kila mwanafunzi anayestahiki kupata mkopo anaupata kwa asilimia zote, ili aweze kusoma kwa bidii na kutimiza ndoto zake.

# Mkurugenzi Mtendaji abanwa ujenzi zahanati

**Na Anthony Ishengoma,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Philemon Sengati, amempa siku saba hadi Septemba 21, mwaka huu, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Emanuel Johnson, kukamilisha ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Mwaweja ili wananchi waanze kupata matibabu.

Dk. Sengati alitoa maagizo hayo jana baada ya kutembelea ujenzi wa zahanati hiyo na kugundua upungufu, hivyo kutoa muda huo kuhakikisha kazi inakamilika na kuanza kupatikana kwa huduma.

Mkuu huyo wa mkoa alishangazwa na hatua ya ujenzi wa zahanati hiyo kuchukua muda mrefu bila kukamilika licha ya fedha kuwapo.

"Zahanati hii ilipaswa kukamilika mwanzoni mwa mwaka huu baadaye ikasimama. Ujenzi wake uliendelea tena na ulitarajiwa kukamilika mwishoni mwa Agosti, ili kuwaondolea usumbufu wajawazito," alisema.

Mzee Frank Shija, Mkazi wa Kijiji cha Mwaweja, alisema kwa muda mrefu wazee kijijini hapo wamekuwa wakishindwa kupata tiba kutokana na kutokuwapo kwa zahanati, hivyo akampongeza mkuu wa mkoa kwa hatua hiyo.

Naye Magreti Kishena akizungumza baada ya agizo la mkuu wa mkoa, alisema kuanza kwa huduma katika zahanati hiyo, kutapunguza adha ya kinamama ambao wamekuwa wakilazimika kukodi mikokoteni kwa lengo la kupata huduma hiyo.

Mbalu Mkinga naye alisema wakazi hao wamekuwa wakisafiri kwenda Kituo cha Afya Ikonda na ili kufika huko mtu anapaswa kuvuka mto na wakati mwingine anaweza kupoteza maisha.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Yudas Ndungile, aliitaka Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu kukamilisha zahanati hiyo ili isajiliwe na kuingizwa katika orodha ya kupatiwa dawa.

HABARI KITAIFA

# Jiji Dar, NBC wawapa elimu wajasiriamali

Na Mwandishi Wetu

HALMASHAURI ya Jiji la Dar es Salaam kwa kushirikiana na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), wameendesha mafunzo ya biashara, elimu ya fedha na mikopo kwa vikundi vya wajasiriamali vijana, wanawake na wenye ulemavu waliopo katika jiji hilo.

Lengo la mafunzo hayo ni kuwaandaa ili waweze kutumia vema mikopo na fursa mbalimbali zinazotolewa na serikali pamoja na jiji hilo.

Akizungumza kwenye mafunzo hayo yaliyowakutanisha pamoja wajasiriamali zaidi ya 400, Ofisa Maendeleo ya Vijana kutoka Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Sapiencia Masaga pamoja na kuipongeza benki hiyo kwa jitihada hizo, alisema mafunzo hayo yatawasaidia kwa kiasi kikubwa wajasiriamali hao kutumia vyema mikopo wanayoipata kutoka serikalini na halmashauri za jiji hilo ili kujikwamua kiuchumi kulingana na malengo ya mikopo hiyo.

"Licha ya jitihada kubwa inayofanywa na halmashauri zetu kwa kutoa mikopo kwa vikundi mbalimbali vya vijana, kinamama na wenye ulemavu bado tumekuwa hatupati matokeo mazuri sana kwa sababu wengi wa walengwa wamekuwa wakishindwa kutumia vema mikopo husika na matokeo yake wanashindwa kufikia malengo na zaidi wanashindwa kufanya marejesho. Tunawashukuru NBC kwa kuwa mafunzo haya yanalenga kuondoa hiyo changamoto," alisema. Meneja Ukuzaji Biashara wa NBC, Isdory Sebastian, alisema benki hiyo imeshirikiana na Halmashauri ya Jiji la Ilala katika kutoa mafunzo hayo ili kujenga uelewa wa kutosha kuhusu usimamizi bora wa kifedha, umuhimu wa bima mbalimbali ikiwamo za afya na biashara pamoja na namna bora ya kutunza akiba zao waweze kuendesha shughuli zao kitaalamu waepukane na hasara inayoweza kukwamisha ustawi wa biashara zao.

"Katika mafunzo hayo Benki ya NBC tumejitahidi kuhakikisha walengwa wanajengewa uelewa wa kutosha ili sisi kama benki tusiishie tu kuwahifadhia fedha zao wanapokopeshwa na hizi halmashauri bali pia tuwasaidie kuhakikisha hiyo mikopo inakuwa na tija kwa pande zote yaani halmashauri na wajasiriamali."

"Tunawashukuru sana Manispaa ya Ilala tungependa na halmashauri nyingine pia waige mfano huu kwa sababu mikopo hii inahitaji elimu sahihi kwa walengwa ili waweze kujikwamua kutoka kwenye umaskini na zaidi pia waweze kurejesha hizo fedha zitumike kuwakopesha wahitaji wengine," alisema.

Wajasiriamali Iddy Kaziulaya na Bahati Angetile walisema mafunzo hayo yatawasaidia kwa kiasi kikubwa katika kuwajengea uwezo wa kibiashara kwa kuwa wengi wao wamekuwa wakishindwa kuendeleza vema mikopo hiyo kulingana na malengo kusudiwa, hali inayochangiwa na kukosekana kwa elimu ya kutosha katika uendeshaji wa shughuli zao.

# Wananchi wahimizwa chanjo ya corona

Na Maulid Mmbaga

WATAALAMU wa afya wameendelea kutoa wito kwa wananchi kuhakikisha kuwa wanapata chanjo ya UVIKO-19 ili kulinda afya zao kwani chanjo ni salama na zinasaidia kuondokana na hali ya hatari pindi mtu anapopata ugonjwa huo.

Hayo yalisemwa na Mhadhiri Mwandamizi kutoka Chuo Kikuu cha Uuguzi cha Rheumatology (University of the West of England, Bristol), Dk. Mwidini Ndosi, alipokuwa akizungumza katika mkutano ulioandaliwa na Shirika la Internews Tanzania na ulihusisha wadau wa afya na wanahabari, ambapo ulifanyika mwanzoni mwa wiki hii kwa njia ya mtandao (zoom).

Alisema utafiti mbalimbali ulifanyika ili kubaini ufanisi wa chanjo zilizopo ikiwamo Johnson & Johnson, Moderna, Pfizer-BioNTech na Oxford-AstraZeneca. Kwa asilimia kubwa zilionyesha kuwa ni salama na huleta unafuu na matokeo chanya kwa mtumiaji dhidi ya UVIKO-19.

"Kuna watu wanauelewa hafifu juu ya elimu ya chanjo ya UVIKO-19, serikali katika baadhi ya nchi za Ulaya na sehemu nyingine ziliwekeza sana katika suala la uelimishaji kwani watu ili waitumie, ni lazima waelimishwe ili kuielewa ndipo waitumie. Pia wataalamu wa afya wanatakiwa kupewa uelewa juu ya chanyo hizo ili watoe huduma yenye ufanisi," alisema Dk. Ndosi.

Aliongeza kuwa kuna baadhi ya taarifa zinasambaa kutokana na matokeo ya chanjo hizo, na alikanusha kuwa baadhi ya kinga hizo zinasababisha ongezeko la nguvu za kiume, na kwamba hazina madhara yoyote katika hilo.

Alisema kuhusu mabadiliko yanayotajwa kujitokeza baada ya kutumia chanjo hizo kwa upande wa wanawake katika mzunguko wa hedhi ni jambo lililoongelewa sana, lakini katika utafiti na wakati wa majaribio haikuonekana kuwa iliwaathiri.

Alisema matokeo ya utafiti kwa waliotumia chanjo zenye dozi mbili kwa wale wenye umri wa miaka 80 na kuendelea, jumla ya watu 156,930 wenye chanjo, kati yao waliopata UVIKO-19 ni 44,590 sawa na asilimia 28.4, na wasiopata ni 112,340 sawa na asilimia 71.6.

"Ufanisi wa dozi hizo ni asilimia 70 kwa ndani ya siku 28-34 baada ya kupata chanjo ya kwanza, na asilimia 89 ndani ya siku 14 baada ya kupata chanjo ya pili.

"Lengo la utafiti ni kujua uwezekano wa kupata maambukizi kati ya watu waliopata chanjo ya Johnson & Johnson na wasiochanjwa, na matokeo tangu Februari 27 hadi Aprili 14, mwaka huu, kati ya kundi la wale waliochanjwa 17,744, waliopata maambukizi ni 128 sawa na asilimia 0.72. Kati ya watu 1,779 waliochanjwa na kufuatiliwa baada ya wiki mbili waliopata maambukizi ni watatu tu, sawa na asilimia 0.17," alisema Dk. Ndosi.

Pia alieleza kuwa kwa mujibu wa takwimu hizo, kuna uwezekano wa maambukizi kupunguzwa kwa zaidi ya mara 4.34, huku ufanisi halisia wa chanjo ukitajwa kuwa ni zaidi ya asilimia 76.7 katika kuzuia maambukizi, na alibainisha kwamba waliochanjwa hubaki na kinga ya ziada kwa zaidi ya asilimia 51 ya kuzuia ugonjwa mkali na kulazwa pamoja na vifo.



Maofisa wa Benki ya NBC wakitoa huduma mbalimbali za kibenki ikiwamo usajili wa akaunti kwa washiriki wa semina fupi ya mafunzo ya biashara, elimu ya fedha na mikopo iliyoandaliwa na Halmashauri ya Manispaa ya Ilala kwa kushirikiana na benki hiyo, ikilenga kuwaandaa wajasiriamali hao kutumia vema mikopo na fursa zinazotolewa na serikali pamoja na manispaa hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC akemea watendaji rushwa, urasimu

Na Richard Makore, MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Robert Gabriel, amewataka watendaji mkoani hapa kuepukana na vitendo vya rushwa na kuondoa urasimu, ili kuwawezesha wawekezaji kufanya shughuli zao bila tatizo.

Akizungumza katika kikao cha baraza la biashara kilichofanyika jana mjini hapa, Gabriel alisema kuna wawekezaji wamewapoteza kutokana na vitendo vya rushwa na urasimu.

"Wakati mwingine mwekezaji anakuja anakutana na ofisa ardhi anampiga cha juu, amvuruge huenda mwekezaji mwingine asikae. Naomba sana watendaji tuwapunguzie mzigo hawa wawekezaji," alisema.

Gabriel aliwahakikishia wafanyabiashara wa Mkoa wa Mwanza kuwa ofisi yake itatumia nguvu zote kuhakikisha wanafanikiwa pamoja na usalama wao na mali zao na kuondoa vikwazo vyote vikiwamo rushwa.

"Ukiona unazungushwa ni dalili za rushwa na rushwa haitakiwa na mlango katika mkoa huu kwa mwekezaji yeyote," alisema Gabriel. Pia alisema wanatakiwa kutumia miundombinu kusafirisha malighafi kutoka mkoani humo kwenda sehemu nyingine kwa lengo la kuleta mapinduzi ya kibiashara.


"Hizi barabara si za kubeba watu pekee, tunahitaji ndege za mizigo zitue na kesho tujue katika reli ya kisasa ni tani ngapi zitawekwa zipelekwe maeneo mengine," alisema na kuongeza kuwa ili uchumi uwe mzuri, wanahitaji shehena za mizigo ambazo zinatoka Mwanza kwenda kwenye masoko mengine.

Alimtaka kila mmoja kutumia kanuni, sheria na taratibu kuhakikisha anawajibika kuweka mazingira wezeshi ya kibiashara. Pia alisema shauku yake kwa mkoa ni kuona unakuwa na mazingira mazuri ya kufanyia biashara.

Naye Mjumbe wa Baraza la Biashara Mkoa wa Mwanza, Dk. Elibariki Mmari, aliomba halmashauri zote kukaa pamoja na wafanyabiashara ili kupanga tozo ya huduma (service levy).

Alisema kwa sasa sheria inataka halmashauri kutoza asilimia 0.3, lakini bado inaonekana ikio juu na kwamba kuna mikoa mingine inatoza chini ya hapo.

Aliongeza kuwa halmashauri ikikaa na wafanyabiashara wanaweza kujipangia wenyewe walipe kiasi gani na kwamba kinachotakiwa na kulipa tozo ambayo haitazidi asilimia 0.3 kama sheria inavyotaka.




Ukurasa 13

Tufuatilie wanetu, lakini kwa umakini



**Ushirika wenye mzizi 1936 unavyodumu kukumbatia tumbaku 'milima, mabonde'**

Ukurasa 14

BUFE
IJUMAA SEPTEMBA 17, 2021
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Nipashe

# Wakagua mzani mpya wa Bn.14/- utakaomaliza foleni ya Namanga

**Novatus Makunga, aliyekuwa Longido**

MKOANI Arusha kuna mradi mkubwa wa ujenzi wa kituo cha mizani cha kupimia uzito wa magari katika barabara kuu ya Tanzania na Kenya, katika eneo la Kimokouwa wilayani Longido. Matarajio ni kwamba utagharimu zaidi ya shilingi bilioni 14

Mizani hiyo ilitarajiwa kuanza kutumika mwanzoni mwa mwezi uliopita, lakini imekwama kutokana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kutotoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT), ambayo ingewezesha kuruhusiwa kutoka katika bandari ya Dar es Salaam.

Kituo cha mizani hiyo, kipo kilomita chache kabla ya kuingia katika Forodha ya Namanga, ambapo ndiyo mpaka wa Kenya na Tanzania na ikiwa miongoni mwa forodha, ambayo inakuwa na shughuli nyingi za kuingia na kutoa bidhaa hapa nchini.

Kwa hivi sasa, eneo hilo linakabiliwa na msururu mrefu wa malori yanayosubiri kupima uzito, kutokana na uwezo mdogo wa mizani uliopo sasa.

Ni changamoto inayomfanya Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Arusha. Zelotte Steven, kufanya ziara mahali hapo na timu yake, ambako walikagua na kutoa maoni ya kinachopaswa kufanyika mahali hapo.

Hapo, Zelote aliyewahi kuwa kamanda wa polisi katika maeneo mbalimbali nchini na kuingia katika siasa alipostaafu, anasema mamlaka husika zinapaswa kuchukua hatua kuhakikisha mzani huo unafungwa haraka, ili kufungua biashara katika eneo hilo la Afrika ya Mashariki.

Kwa mujibu wa nyendo za kiutendaji ndani ya CCM, imekuwa ikichukua hatua za kufanya ziara kukagua miradi ya umma, ikiwa ni usimamizi wa utelezaji wa ilani ya serikali inayoiongoza.



Mizani ya Kupima Uzito wa Magari, Longido, Arusha. **PICHA: NOVATUS MAKUNGA**

Ikirejewa mradi wa Mizani tajwa, mamlaka zinazotajwa zinajumuisha Wizara ya Fedha na Mipango, kwa maana wasimamizi wa TRA na Wizara ya Ujenzi wanaosimamia Wakala wa barabara Tanzania (Tanroads), ambao ndiyo wenye mizani.

Hadi sasa miongoni mwa hatua za ugumu katika kusimamia nyendo za ukuaji biashara katika eneo la Afrika ya Mashariki, unatajwa kuwapo vikwazo visivyokuwa vya kodi.

Ni hatua inayogusa maeneo kama ya urasimu mkubwa katika barabara zinazounganisha nchi hizo, hasa kuwapo mizani mingi na vituo vya polisi vya kukagua magari.

Kunatajwa kuwapo ucheweleshaji wa usafirishaji mizigo katika barabara, hata ikaongezea gharama wasafirishaji wanaokaa muda mrefu barabarani, kabla ya kufika wanakoelekea

Katika maeneo ya mizani, madereva nao wanatumia kati ya dakika 10 mpaka 30, kukamilisha taratibu za kupima uzito wa magari yao.

Lakini, kunatajwa mizani mingine inayokabiliwa na misururu mirefu ya magari, inayowafanya madereva kutumia muda mrefu hadi kufanikiwa kuvuka mizani, hali inayochangia hata kuongeza gharama za usafiri na usafirishaji

Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EAC), ilianzisha Umoja wa Forodha mwaka 2005 na baadaye Soko la Pamoja mwaka 2009 kwa lengo la kurahisha usafirishaji wa bidhaa na huduma, pia kurahishia usafiri wa wananchi katika eneo hilo, kutoka nchi moja kwenda nyingine

Inatambulika vikwazo hivyo, ambavyo siyo kwa kodi, mara zote huwekwa, kwa sababu za msingi zikiwamo: Kulinda afya na usalama wa binadamu wanyama, mimea na mazingira, kulinda viwanda vya ndani na walaji wake, kulinda usalama wa nchi na ulinzi, pia namna bora ya kukusanya mapato

Kuna lingine, suala la kuhakikisha barabara kubwa zinakuwa na vitendea kazi vya kisasa vitakavyopunguza gharama za usafirishaji bidhaa ni la muhimu, ukiwamo mzani wa forodha uliopo Namanga.

Takwimu zinaonyesha katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, kuna jumla ya malori 1,268 yaliyosafirisha bidhaa kwenda nchi jirani ya Kenya, kupitia mpaka huo, yalikuwa huku mauzo ya bidhaa, ambazo zinapitia Namanga zikiwa na thamani wastani wa shilingi bilioni 25.1, kwa mwezi.

Bidhaa za viwandani zinazoongoza kwa mauzo ya nje kupitia mpaka wa Namanga, ni pamoja na vigae vya sakafuni na ukutani kutoka Mkuranga mkoani Pwani.

Bidhaa nyinginezo zinazong'ara kwa mauzo kupitia mpaka wa Namanga, pia kuna vinywaji vikali, vya matunda na vya kuongeza nguvu, unga wa ngano na sembe.

Orodha, inagusa pia mboga, mashudu ya pamba, tangawizi na madini ya viwandani, yakiwamo makaa ya mawe na chokaa.

UCHUMI

# Kilimo mboga 'kinavyowatoa' kinamama wanaoelemewa na maisha duni, uonevu

## • Rasmi wahamia paliposheheni raha kifamilia

**Na Shaban Njia, KAHAMA.**



Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, akiwa na ndoo ya nyanya zilizovunwa katika shamba la kikundi cha LumoLumo, alipozindua Siku ya Mkulima katika Kata ya Segese, Halmashauri ya Msalala. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA.**

ASILIMIA kubwa ya wananchi wanaoishi pembezoni mwa miji wamekuwa wakijikita kwenye shughuli ya kilimo cha mazao ya biashara na kujiingizia kipato, kinacho tumika kuendesha familia zao, ikiwamo kusomesha watoto.

Katika Wilaya ya Jahama, wananchi wake wamejikita katika uzoefu wa muda mrefu, katika kilimo cha tumbaku, pamba, mpunga, mahindi, dengu na choroko, asilimia kubwa mazao hayo, yanaliwa ndani ya Halmashauri za Ushetu, Msalala na baadhi ya maeneo ya Halmashauri ya Manispaa ya Kahama.

Takwimu ya wakulima wa mazao ya kibiashara tumbaku na pamba jumla yao wako 11,890, huku wanaolima tumbaku jumla yao ni 5090.

Wakulima wa pamba walikuwa ndio wanaolima mazao mengine ya kibiashara, ikiwamo mpunga, mahindi, dengu na choroko.

Hivi sasa katika maeneo hayo, shirika lisilo la kiserkali linalojishughulisha na kilimo cha mboga na matunda (TAHA) linaloendesha mradi wa kutambua usawa wa kijinsia, kwa kuwawezesha wanawake na mabinti katika kilimo cha mboga, ili wajikwamue kiuchumi.

Mradi huo unatekelezwa na shirika hilo kwa ufadhili wa asasi ya UN-Women na KOICA, ndani ya Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, hilo, likifanywa katika Kata za Segese, Lunguya na Kijiji cha Malito.

Ni njia inayotumika kukabili matukio ya ukatili, dhidi ya wanawake na wadau kutoka China, wanaokabili tatizo la utapiamlo na udumavu.

Kilimo cha mboga mboga na matunda, Halmashauri ya Msalala, mkoani Shinyanga, imeleta matumaini mapya kiuchumi kwa kikundi cha ujasiriamali kinamama Lumolumo, kuondokana na utegemezi kwenye familia na kupigwa na wanaume zao, wanapochelewa kurejea nyumbani.

### WANAWAKE LUMOLUMO

Angela Paul, Makamu Mwenyekiti wa kikundi Lumolumo anasema, elimu ya kilimo cha mboga na matunda kinaleta matumaini ndani ya familia na kuwainua kiuchumi waondokane na maisha ya utegemezi ndani ya familia na mabinti wanaoshinda mitaani, bila shughuli ya kufanya.

Anasema, kabla ya kupewa elimu ya kilimo cha mboga na matunda, walikuwa tengemezi kwenye familia zao na kuna wakati ilifikia hatua ya kupigwa na waume zao walipochelewa kurejea majumbani mwao, kwa sababu hawakuwa na shughuli ya kufanya.

Makamu Mwenyekiti huyo, anasema kwa sasa wanaheshimika kwenye familia, baada ya kupata shughuli ya kufanya na kujiingizia kipato cha kaya, hata wakichelewa kurejea majumbani, hakuna mafarakano baina yao.

"Halmashauri hii inazaidi ya vijiji 92 na vijiji vinne ndivyo vinavyonufaika na mradi huu. Tunaomba elimu tuliyoipata iwafikie na kinamama na mabinti wengine, ili kuwakwamua kiuchumi na kupunguza wimbi la mabinti wasiokuwa na shughuli za kufanya mitaani," anasema Angela.

Mhasibu wa kikundi hicho, Edina Shigela, anasema wamelima shamba ukubwa ekari moja ya nyanya na matunda aina ya pasheni, wakiwa na matarajio watakapovuna wanatarajia kupata si chini ya Sh. milioni 20 na kuendelea ili kujikwamua kiuchumi.

Hata hivyo, anasema kwa fedha ambazo wamekuwa wakizipata shambani, wanatarajia kununua gari ua bajaji, kwa ajili ya kubeba mazao yao na hasa nyanya shambani, kwa ajili ya kuzipeleka sokoni na wataendelea kuzalisha kwa kiwango kinachohitajika, ili kuendelea kupata soko la uhakika.

### SOKO LA MAZAO

Makamu Mwenyekiti Angela, anasema licha ya kuanzisha kilimo hicho, hawana ugumu wa masoko, kwa sababu wateja ni wengi wa kutosha wanaofika kununua bidhaa zao na kuchukua mzigo, ukiwa bado shambani kabla ya mavuno.

Anatoa rai ya kupatiwa elimu ya kusimamia mazao, kuanzia wanapopanda mpaka kuvuna, ili yasiharibike na hata wakapata hasara, kwa sababu wanatumia gharama kubwa kuwekeza shambani.

"Tunahitaji tuelekezwe namna bora ya kutumia viatilifu kwenye mimea hasa nyanya, ili kudhibiti uharibifu pindi ugonjwa wa nyanya unapojitokeza sambamba na elimu ya kuzitambua mbegu bora, ambazo wakizitumia kwenye uzalishaji zitaleta tija." anasema Agela.

### WADAU SHAMBANI

Mkurugenzi wa shirika lisilo la kiserikali la Kilimo cha Mboga na Matunda (TAHA) Dk.Jackline Mkindi, anasema wameanzisha mradi huo katika Halmashauri za Ikungi, mkoani Singida na Msalala wilayani Kahama mkoani Shinyanga, lengo

ni kupambana na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na wasichana.



Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, akichuma nyanya katika shamba la kikundi cha Lumolumo kinachojihusisha na ulimaji mboga na matunda.

Anasema kinamama na mabinti wamekuwa wakifanyiwa vitendo vya kikatili ndani ya familia na nje, kwa sababu za kiuchumi, akikiri kilimo cha mboga na matunda kinawasaidia kujikwamua kiuchumi na kukabili utapiamlo.

Dk. Mkindi ana rai kwa vikundi vingine kujitokeza kujifunza kilimo cha kisasa cha matunda na mboga, kujikwamua kiuchumi, wakijiengua na maisha hodhi ya utegemezi kwenye familia zinazowapatia lishe kamili watoto wadogo.

Anasema, licha ya elimu wanayoitoa, wanawatafutia masoko ya kuuza mazao yao, hivyo kikundi hicho kinatarajia kupata soko la uhakika la mazao yake, kupitia umma wa migodi miwili jirani ya Bulyanhulu na Buzwagi na kuwataka kuendelea kuzalisha kwa viwango vinavyohitajika, ili kukidhi mahitaji ya soko.

Mratibu wa asasi ya Umoja wa Taifa inayoshugulika na Wanawake (UN-Women), Lilian Mwamdanga, anasema lengo la kuwapatia ujuzi wanawake na mabinti kulima bustani za mboga na matunda, ni kuboresha maisha yao, wakienguliwa kutoka ukatili wa kijinsia na utapiamolo uliokithiri kwa watoto.

Anasema, tatizo la utapiamlo na udumavu kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano limekuwa tatizo linalohitaji nguvu ya ziada kulitatua, hivyo mbali na utaoji elimu ya kilimo hicho, wanaenda sambamba na utoaji wa elimu ya maandalizi ya chakula chenye lishe.

### DC KAHAMA

Festo Kiswaga, ni Mkuu wa Wilaya ya Kahama, anayesema kuwa, kwa kuona umuhimu wa kilimo ameagiza wenyeviti wa vijiji na kata kuorodhesha vijana wenye umri kuanzia miaka 14 na kuendelea, ambao sio wanafunzi na kuhakikisha wanalima ekari sita za mazao ya pamba, tumbaku na choroko.

Anasema, anapohamasisha kilimo cha mazao hayo anamaanisha, kwa sababu msimu uliopita binafsi alilima mazao ya kibiashara na kupata magunia 600 ya mahindi na magunia 1000 ya mpunga,

Kupitia tendo hilo, anasema anamaanisha azma yake, kwa maana ya kulima mazao hayo sio ombi, bali ni lazima kwa kila kijana mwenye umri huo.

"Wakati nikiwa Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, nimekuta wanazalisha pamba kilo milioni 20. Tulikaa tukazungumza na tukakubaliana msimu uliofuata tukazalisha kila milioni 35 na mpaka nahamia hapa Kahama nimeacha wanazalisha kilo milioni 51. Hivyo, hapa kwetu niliyoyasema yanawezekana," anahamasisha Kiswaga.

Pia, anawataka watendaji wa vijiji kuorodhesha majina ya vijana hao kila kaya na kuwasilisha ofisini kwake, kwa ajili ya maandalizi ya kuwapatia pembejeo na dawa bure kwa ajili ya kilimo, isipokuwa kilimo cha choroko ndio itawalazimu kununua pembejeo.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Tufuatilie wanetu, lakini kwa umakini






NA JOSEPH KULANGWA
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
jkulangwa@yahoo.com

NI jambo la kawaida na si nadra kukuta mwalimu akimfundisha mwanafunzi, ambaye baadaye anakuja kumzidi mwalimu wake.

Hivyo si jambo la kushangaza kukutana na mwanafunzi, ambaye ana mafanikio makubwa kuliko mwalimu wake. Tulishashuhudia marais wanaotafuta walimu wao kuwashukuru.

Mwanafunzi mwerevu ni anayefuatilia mafunzo anayopewa na kuja kufanikiwa baadaye, kutokana na mafunzo hayo. Wapo wanaoshukuru, lakini wapo pia wasiofanya hivyo, wakisema ni wajibu wa mwalimu.

Duniani kuna nchi, ambazo wanafunzi wa nchi zingine na ndizo zimeonekana kuwa walimu wa nchi wanafunzi, zinazokuja baadaye kufanikiwa na kupata maendeleo makubwa kuliko hata walimu.

Rwanda ni mwanafunzi mwerevu aliyefundishwa na mwalimu Tanzania na sasa ni Taifa linalopata maendeleo kwa kasi kubwa. Kuna Wanyarwanda wengi walioishi Tanzania ama kwa kuhamia tu au kukimbia.

Waliishi wakajifunza mengi na waliporejea kwao, wakayatumia mafunzo hayo kikamilifu kuijenga nchi yao na sasa wanashuhudia mafanikio, ambayo msingi wake ni Tanzania.

Kuna maprofesa waliosoma na kufundisha Tanzania na waliporudi kwao wakatumia usomi wao kuibadilisha nchi yao. Ukitaka kuwaona nenda KIST, pale Kigali, hiki ni chuo au Taasisi ya Sayansi na Teknolojia. Walikuwapo.

Huko nyuma Tanzania tulikuwa na sera nzuri na madhubuti za kujijenga, bahati mbaya nyingi zikabaki vitabuni, huku wenzetu wa Rwanda wakizichukua au kuzikopa na kuzifanyia kazi. Leo kwa sera hizo hizo wako mbali.

Ni wanafunzi waliofundwa Tanzania na sasa wamefanikiwa maradufu kumtikisa mwalimu huyo. Sasa tunakwenda kujifunza Rwanda, yale ambayo tulipaswa kuwa nayo huko nyuma mapema kabisa.

Rwanda hivi sasa wanaumba magari, namaanisha kuunganisha, tusingeua magari ya Nyumbu na sisi Watanzania leo tungekuwa wapi? Tungeagiza hata Power Tiller Ughaibuni kweli? Tungeagiza pikipiki? Hata baiskeli kweli?

Angalia Wanyarwanda, hivi sasa wanatumia ndege zisizo na rubani kusafirishia vifurushi kwa maana ya hizo mnazoita 'drones'. Wanapeleka dawa na vitu vingine kwa ndege hizo, kutoka sehemu moja kwenda nyingine, bila ya gharama kubwa.

Hivi sasa tunakwenda Rwanda kujifunza jinsi ya kukagua wanafunzi wetu wanafundishwa nini kwenye madrasa na shule za Jumapili! Tunakwenda Rwanda kujifunza jinsi ya kufundisha uzalendo shuleni!

Hata hivyo, si jambo baya kufanya hivyo, kwa sababu suala la msingi ni kuhakikisha watoto wetu wanakuwa katika maadili mema na uzalendo na kuepuka kuwaingiza katika mafunzo yatakayowaharibia mustakabali wa maisha yao na Taifa.

Lakini, ni vizuri kulifanya hili kwa umakini mkubwa, tusijejikuta tumekosea na kutisha watoto wetu na ugaidi ambao wengi kwa umri wao hawaujui. Tunaweza kuwa na nia njema, lakini ikatutumbukia nyongo katika baadhi ya magumu.

Mathalan, inapotokea jambo la kishule, inapendeza zikaenda mamlaka za kitaaluma na si zinazofanana nguvu za dola. Tunaweza kukagua mihutasari yao na kama ni lazima, wakaenda wakaguzi wa elimu,

Sawa, yawezekana majirani hao wakawa wamefanya hivyo na kufanikiwa, lakini idadi yao ni ngapi? Ukubwa wa nchi hiyo ukoje? Kama tunaweza kulifanya hili, je ni hilo tu tulilojifunza kwao?

Katika baadhi ya nyumba za ibada zlipochipua kama uyoga kila kona ya nchi, wenzetu hawakuangalia makunyanzi, wakawa wamefunga baadhi yao. Yakabaki makini na si kila alalaye na kuamka, anaibuka na lake akijipa jina kubwa.

Hapa kwetu tulishashuhudia baadhi ya matukio ya kijamii yaliyowaacha baadhi kwenye butwaa dhidi ya ushuhuda wa ya hatari.

Kama kweli tunataka kupandikiza na kudumisha uzalendo kwa wanetu, basi yatupasa pia kuangalia uyoga huu wa yasiyofaa.

Angalau katika baadhi ya maeneo ya imani, huko kwa majirani haamki mtu akajenga kizimba hicho cha imani na kuhubiri, kwa namna anavyojua yeye pekee. Hapo ndipo najiuliza, hao wanaojenga na kusambaza, kulikoni?

Tupitie kwa umakini maeneo haya tukufu kiiimani, yakabaki yanayonufaisha umma kiimani, na si yenye sura ya maslahi binafsi, kwa sababu yanatuchanganya. Tumeshuhudia wenyewe mbona!

Tubaki na yanayutufundisha neno sahihi na si yanayofundisha mifarakano, kwa kuchanganya na mambo mengine yasiyo na ustawi kijamii. Au hatuyaoni? Tukifanya hayo, bila shaka hatutatumia nguvu kubwa kwa wanetu. Alamsiki!

BIASHARA

# Ushirika wenye mzizi 1936 unavyodumu kukumbatia tumbaku 'milima, mabonde'

- Kiulizo; Uzalishaji tani 500 kutoka 10,000
- Vita sasa soko la mbaazi kuvuna pesa India

**Na GIDEON MWAKANOSYA, SONGEA**

CHAMA kikuu cha Ushirika cha mkoani Ruvuma au 'SONAMCU LTD' kiliandikishwa mnamo Januari 30, mwaka 2003.

Lakini, inapochimbwa zaidi ilitokana na vyama vikuu vya ushirika tangulizi vitatu, mojawapo kikiwa mzizi mrefu wa uasisi, leo hii inatinga miaka 85.

Hiko ni Ngoni Matengo Tobacco Growers Cooperative Union (NGOMAT) kilichoanzishwa mwaka 1936, ambacho miaka 18 iliyopita, iliungana na Songea Agricultural Cooperative Union (SAMCU) cha mwaka 1994 na Ruvuma Cooperative Union (RCU), kilichoasisiwa mwaka 1989.

Chama hicho kikuu kina wanachama wa vyama vya msingi, kati yao 35 ni kutoka Wilaya ya Namtumbo; vitano Songea Vijijini; viwili vinatoka katika Manispaa ya Songea; vyama vitatu kutoka Mbinga Vijijini; na kimoja Madaba.

Meneja wa SONAMCU, Juma Mwanga, anaeleza kuwa Chama hicho kilianzishwa kwa lengo la kusimamia na kuratibu masoko ya tumbaku na mazao mchanganyiko, yaliyoko wilayani Namtumbo na Songea, pia uendeshaji wa shughuli za kila siku za vyama vya msingi (Amcos).

Mengine kwa mujibu wa meneja huyo, ni kutoa elimu ya ushirika na ujasiriamali kwa vyama hivyo vya msingi wanachama wake, huku ikizitafutia masoko ya nje ya nchi ya mazao ya vyama wanachama.

Wakati huohuo, Mwanga anasema wanahamasisha wakulima wao kukusanya na kuuza mazao yao kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani na kuwapa mikopo midogo wanachama wamudu kuendesha shughuli zao.

Anasema, chombo chao kinaendeshwa kwa kutekeleza yaliyoamuliwa na mkutano mkuu unaoiachia bodi kusimamia menejimenti katika shughuli zao za kila siku.

**MALI ZAKE**

Chama Kikuu cha Ushirika - SONAMCU kinamiliki mali mali zake kwa asilimia 100, ambazo meneja wao Mwanga anaorodhesha baadhi kuwa ni kiwanda cha tumbaku, hoteli ya Angon Arms, maghala, Chuo cha Ushirika na majengo mbalimbali

Anasema, katika kuhakikisha chama kinajiendesha pasipo kutegemea ushuru utokanao na mauzo ya mazao ya wakulima, kimeweka mikakati mbalimbali

Mojawapo ni kiwanda cha vifungashio kinachojengwa wilayani Namtumbo, kukiwapo matarajio ya kuajiri watumishi 500, kitakapoanza kafanya kazi mwanzoni mwa mwaka ujao.

Anaendelea: "Katika mwaka wa fedha 2022/2023, chama kina mpango wa kununua na kuanzisha mashamba yenye ukubwa wa ekari 3,000, mashamba ambayo yatatumika kwa shughuli za kilimo hasa yale yanayouzwa kupitia mfumo wa Stakabadhi Ghalani, yaani (mazao) ufuta, soya na mbaazi."

Mpango mwingime anautaja kutafuta masoko ya ziada ya zao tumbaku, kwani kwa uzalishaji tumbaku ni tani 500 pekee, wakati uwezo uliopo ni kulima zaidi ya tani 10,000.

Hadi sasa, Mwanga anasema wanashirikiana na Ofisi ya Bodi ya Tumbaku Tanzania, kujadili namna ya kutafuta wanunuzi wengine wa tumbaku, badala ya kutegemea mnunuzi mmoja, kampuni ya Premium Active Tanzania.

Kwenye mwaka wa fedha 2022/2023, chama kinanuia ama kukodisha au kutafuta mbia wa kuendesha miradi yake iliyosimama, kama vile hoteli ya Angon Arms na Chuo cha Ushirika, kilichopo wilayani Namtumbo.

Akielezea kuhusu mpango wa Stakabadhi Ghalani alisema kuwa mkoa wetu wa Ruvuma uliingia katika mfumo wa Stakabadhi ghalani mnamo mwaka 2019.

Baada ya kupokea waraka wa mrajis wa vyama vya ushirika Tanzania mnamo mwaka 2019. Hivyo chama kilipokea mwongozo kutoka ofisi ya mkuu wa mkoa juu ya usimamizi na uratibu wa masoko ya mazao ya ufuta, soya na mbaazi.

**STAKABADHI GHALANI**

Mwanga anaeleza mafanikio waliyoyapata kupitia mfumo huo wa stakabadhi ghalani, wakulima kwa sasa wanakutanishwa na wanunuzi kuwafanya wawe na uamuzi katika uuzaji mazao yao kupitia umoja walio nao.

Hadi sasa kuna manufaa yanayotajwa ya Stakabadhi Ghalani, kama vile matumizi ya vipimo, kama vile mizani iliyohakikiwa na wakala, badala ya majagi yaliyotumika awali.

Pia, serikali inanufaika kirahisi katika kupata hisa yake ya tozo za ushuru kirahisi, ikilinganisha kabla ya mfumo huo, huku kukishuhudiwa kuongezeka bei za mazao kama ya ufuta, soya na mbaazi kwani wanunuzi wameshindanishwa bei.

Mengonwe ya manufaa, vyama vya ushirika vimefufuka kutoka 24 vilivyokuwa vinauza tumbaku na sasa vimehamasika na kukwea hadi idadi 63 vikifikia mazao kama ufuta, soya na mbaazi, sababu kuu ni uhakika wa masoko.

**VIKWAZO SHAMBANI**

Meneja wa chama hicho kikuu cha ushirika, anataja kuwa ni sehemu ya magumu kwao, ikiwamo kukosekana elimu ya stakabadhi ghalani kwa wakulima hasa katika maeneo ya wilaya za Nyasa, Mbinga na Madaba.

Lingine analodokeza ni kuongezeka misuguano ya kimaslahi kwa wafanyabiashara wanaopinga mfumo kutumia wanasiasa, hapo maslahi ya ugumu ni kuwapo udhibiti wa utoroshwaji mazao nje ya mfuko wa stakabadhi ghalani.

Pia, inatajwa uwapo wa miundombinu isiyo rafiki na hasa barabara katika baadhi ya maeneo. Hiyo inatajwa imewafanya wakulima washindwe kufikisha mazao yao sokoni kirahisi.

Mkanganyiko mwingine unaotajwa kuzua mgogoro katika ushiriki mkoani Ruvuma, unatajwa ni mabadiliko mengi ya matamko ya viongozi wa juu ya ghafla kuhusu Mfumo wa Stakabadhi Ghalani, ikichangia kukosekana uhakika wa maandalizi ya soko msimu unaofuata.

**KUSHUKA TUMBAKU**

Meneja wa Ushirika - Mwanga, anasema kupungua uzalishaji tumbaku nchini kutoka tani 9000 za mwaka jana, hadi 500 mwaka huu, inatokana na Tanzania kujitoa uanachama wa jumuiya ya COMESA, huku mteja mkuu wa Tumbaku ya mkoani Ruvuma ni taifa la Misri.

Sasa kutokana na hali hiyo, rai yake ni kwamba serikali ya mkoa kwa kushirikiana na Bodi ya TumbakuTanzania (TTB), iwasaidie kupata wanunuzi wa zao hilo, ili kuongeza uzalishaji kimkoa.

Pia, ana ombi kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, akiongezea msisitizo wa kuimarishaa mfumo wa Stakabadhi Ghalani, kwani umeleta tija kwa wakulima wa mkoa Ruvuma.

"Tunaiomba serikali kupitia wizara ya kilimo kuingia mkataba wa muda mrefu na nchi ya India juu ya uuzaji wa zao la mbaazi, ili kuwafanya wakulima mbaazi wawe na uhakika wa soko," anasema.

- **Mwandishi wa makala anapatikana kupitia simu:+ 255 715-928752**



Zao la ufuta, ambalo limo katika orodha yanayouzwa kupitia mfumo Stakabadhi Ghalani..



Meneja wa Ushirika SONAMCU, Juma Mwanga. **PICHA ZOTE: GIDEON MWAKANYOSA.**

Zao la
mo katika
uzwa
Stakaba-



## HABARI DODOMA

# Mwongozo kuzibana asasi zinazofaidika kupitia wenye ulemavu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, amesema mwongozo wa kitaifa wa utoaji huduma kwa watu wenye ulemavu utazibana asasi ambazo zimekuwa zikinufaika kupitia mgongo wa watu hao.

Aidha, amepongeza Taasisi ya Dk. Mengi Foundation kutokana na kuwa mstari wa mbele kwenye masuala ya watu wenye ulemavu.

Mhagama alitoa kauli hiyo jana kwenye mkutano wa wadau kuhusu masuala ya utoaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu, uliofanyika jijini hapa.

Alisema kuna baadhi ya asasi zimejipambanua.

"Mwongozo huu unatoa utaratibu kwa wadau katika kuandaa afua mbalimbali za watu wenye ulemavu, bila asasi kutumia manufaa yao kwa jina la watu wenye ulemavu, ipo shida ya baadhi ya asasi zinabeba majina ya watu wenye ulemavu kwa kujinufaisha wao wenyewe," alisema.

Alisema mwongozo huo utaweka utaratibu wa asasi na afua zote zinavyojipambanua kushughulikia kero za watu wenye ulemavu ili zishughulikie kweli kero hizo na si kwenda kufaidisha matumbo ya watu binafsi.

"Yaanishwe maeneo ya kipaumbele yanayopaswa kutekelezwa na wadau wote ikiwamo serikali tunataka kuwa na ujumuisha uliotimilifu wa watu wenye ulemavu katika shughuli zote nchini na uainishe hatua mahsusi za kuimarisha huduma bora zinazotolewa kwa watu wenye ulemavu nchini," alisema.

Kadhalika, alisema mwongozo huo utatoa msisitizo juu ya uwepo wa afua zinazotambua kwa mapana na mgawanyo sawa unaendana na mahitaji halisi ya maeneo mbalimbali nchini kutokana na baadhi ya asasi kukimbilia maeneo ya mijini hasa miji mikubwa.

"Vilevile tofauti na miongozo mingine ya awali, mwongozo huu unakusudiwa kuwa wa muda mrefu unaoweka na kutoa dira na mwelekeo wa vipaumbele muhimu vya kitaifa katika ujumuishwaji, utoaji na upatikanaji wa huduma bora kwa watu wenye ulemavu nchini," alisema.

Naye, Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, Ummy Nderiananga, alisema lengo ni kupata maoni ya wadau ya kuboresha mwongozo huo na watajadili kuhusu afua zinazotolewa na serikali na wadau kwa watu wenye ulemavu nchini.

Alisema Sh. bilioni 1.2 zimetengwa katika bajeti ya mwaka huu 2021/22 kwa ajili ya masuala ya watu wenye ulemavu.

"Ajira 381 za watu wenye ulemavu zimepatikana haijawahi kutokea, vijana wenye ulemavu 374 wameingizwa kwenye programu ya uanagenzi," alisema.

Alisema ofisi hiyo ipo hatua za mwisho kukamilisha mwongozo huo kwa kusaidiwa na Shirika lisilo la kiserikali la CBM.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu, Ernest Kimaya, aliishukuru serikali kwa kuwajali watu wenye ulemavu hususan kwenye ajira za walimu zilivyotoka hivi karibuni ambapo jumla ya walimu 387 wamepata ajira.

# Serikali yazindua mfumo kijiditali huduma za afya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, amezindua mfumo wa kidigitali wa usimamizi shirikishi kwenye huduma za afya (AfyaSS) na kugawa vishikwambi 900 ili kutatua kero mbalimbali zilizopo kwenye sekta ya afya.

Mfumo huo umetengenezwa na wizara hiyo kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Shirika lisilo la kiserikali la PATH kupitia mradi wa 'Data use partnership'.

Akitoa maelezo ya mfumo huo jana kwenye Mkutano Mkuu wa Waganga Wakuu wa mikoa na halmashauri nchini, Mkuu wa kitengo kidogo cha usimamizi shirikishi wa wizara hiyo, Dk. Chrisogone German, alisema kupitia mfumo huo utarahisisha uratibu na usimamizi wa shughuli za sekta ya afya, matumizi ya takwimu na ufuatiliaji wa mipango inayotekelezwa.

"Tumenunua vishkwambi 900 ambavyo tutavigawa kwa Halmashauri na mikoa ambapo kwa kila mkoa vishikwambi vitatu na kila halmashauri vishkwambi vitatu, tumetoa mafunzo kwa watumishi ngazi mbalimbali, hii itasaidia uratibu mzuri na kuokoa rasilimali," alisema.

Alibainisha kuwa katika mfumo huo wanatarajia kutakuwa na uratibu mzuri, upatikanaji wa taarifa kutoka ngazi zote kuanzia kwenye vituo, ufuatiliaji wa mipango kazi kwenye vituo na kupunguza gharama za usimamizi.

"Kwa mantiki hiyo kutokana na mfumo huu tunategemea kwamba zitarahisisha suala la usimamizi shirikishi katika sekta ya afya, tutaendelea kutoa mafunzo kwa Wizara ya Afya na OR-TAMISEMI ambao mpaka sasa tuna wakufunzi wa kitaifa 28 ambapo 22 kutoka Wizara ya Afya na sita kutoka OR-TAMISEMI," alisema.

Alisema kwa upande wa mikoa wamefundisha wakufunzi 52 kutoka mikao yote ambao ni Waratibu wa Uimarishaji wa Ubora wa Huduma na Waratibu wa MTUHA.

"Tunachangamoto kidogo kwenye suala la kusambaza mfumo tunatarajia baada ya mfumo kuzinduliwa rasmi tutaanza kuongea na wadau ili waweze kusaidia kusambaza mfumo katika mikoa na halmashauri.

Kwa kutumia wale wakufunzi ambao tumewafundisha kwenye mikoa husika wataanza suala la kusambaza mfumo kwa kutumia wadau walipo mikoani au kwa kutumia bajeti zetu za ndani," alisema.



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima (kushoto), akipokea zawadi ya kava la tairi ya gari lenye ujumbe maalum wa kuhamasisha chanjo ya UVIKO-19 kutoka kwa Mkurugenzi wa Huduma za Afya wa Taasisi ya Christian Social Services Commission (CSSC), Dk. Josephine Balati alipotembelea banda la taasisi hiyo, wakati wa mkutano wa waganga wakuu wa mikoa jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Tahadhari kuingiza bidhaa za mitumba zinazotumia gesi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imewataka wananchi kuepuka kuingiza gesi nchini zilizopigwa marufuku na vifaa vinavyotumia gesi haribifu ikiwamo majokofu na viyoyozi vya mitumba ili kulinda tabaka la Ozoni.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, alibainisha hayo jana jijini hapa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni.

"Septemba 16, mwaka huu, tutaungana na jumuiya ya kimataifa kuadhimisha siku ya kimataifa ya hifadhi ya tabaka la Ozoni kama ilivyoagizwa na makutano mkuu wa Umoja wa Mataifa katika azimio lake namba 49/114 la tarehe 19, Desemba 1998," alisema Jafo.

Jafo alisema, tabaka la Ozoni linapoharibiwa huchangia kuruhusu mionzi zaidi kufika kwenye uso wa dunia na hivyo kusababisha kuongezeka kwa magonjwa kama vile saratani ya ngozi, uharibifu wa macho yaani mtoto wa jicho unaosababisha upofu.

"Pia husababisha upungufu wa kinga dhidi ya maradhi na kujikunja kwa ngozi," alisema Jafo.

Kadhalika, alisema madhara mengine ni kuharibika mimea hasa mazao ya kilimo kutokana na kuathirika kwa maumbile na mifumo ya ukuaji.

"Vilevile baadhi ya kemikali hizi husababisha kuongezeka kwa joto duniani na hivyo kuchangia katika mabadiliko ya tabianchi," alisisitiza waziri huyo.

Alisema ili kulinda tabaka hilo serikali za mataifa mbalimbali zilikubaliana kuunda mkataba wa Viena wa hifadhi ya tabaka la Ozoni mwaka 1985.

"Mkataba huu unasisitiza ushirikiano katika utafiti usimamizi na ubadilishanaji wa taarifa za hali za tabaka la Ozoni kutokana na kupungua kwa matumizi yake," alisema.

Alisema pia ilianzishwa Itifaki ya Montreal inayohusu udhibiti wa kemikali zinazomong'onyoa tabaka la Ozoni.

Alisema ili kudhibiti hali hiyo serikali pia inasisitiza kuingiza nchini vipoozi mbadala na rafiki kwa tabaka la Ozoni kama vile R209, R407, R404 na R717.

"Pia kununua bidhaa zilizowekwa nembo rasmi isemayo 'Ozone friendly' yaani Sahibu wa Ozoni au CFC-free ikiashiria haina wala haikutengenezwa na kemikali zinazomong'onyoa tabaka la Ozoni," alisema.

Jafo, alisema wananchi wanatakiwa kuepuka kutupa ovyo majokofu ya zamani ama vifaa vya kuzimia moto vyenye kemikali zinazomong'onyoa tabaka la Ozoni aina ya CFCs na halon.



# Mil. 400/- zatengwa ujenzi kituo cha afya

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya kupitia mapato yake ya ndani, imetenga Sh. milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Ngonga ambacho pia kitatoa huduma ya mama na mtoto.

Lengo la ujenzi wa kituo hiki ni kuwasaidia wajawazito na watoto kupata huduma kwa karibu. Kwa sasa wananchi waaohitaji huduma hutumia muda na gharama kubwa kuzifuata katika Hospitali ya Wilaya hiyo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Katule Kingamkono, alisema juzi kuwa walikubaliana kujenga kituo hicho cha afya baada ya kuona madhila wanayopata wananchi wa Kata za Ngoja, Katumba Songwe na Ikolo katika kupata huduma bora za afya.

Alisema kituo hicho kitahudumia zaidi ya wakazi 10,000 ambao watanufaika na huduma bora za matibabu baada ya kukamilika.

"Halmashauri ya Wilaya kupitia mapato ya ndani, tumetenga Sh. milioni 400 pamoja na eneo kubwa ambalo litajengwa kituo kikubwa cha afya kitakachohudumia wakazi wa Ngonga na maeneo jirani katika bajeti yetu ya mwaka 2021/2022.

"Naamini ndani ya mwaka huu tutafikia hatua nzuri na ikiwezekana kumaliza kabisa kadri fedha zitakapopatikana pia tunawakaribisha wadau kusaidia," alisema Kingamkono.

Aliongeza kuwa katika kuboresha huduma za afya, serikali kuu imetoa Sh. milioni 550 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Itunge na Zahanati ya Kilasilo.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Ismail Mlawa, aliwataka madiwani kusimamia vyema miradi ya maendeleo, ili wananchi wapate huduma bora na za uhakika.

Alisema Wilaya ya Kyela ni kongwe, lakini haisongi mbele kwa sababu ya kukosa uzalendo, hivyo akawashauri viongozi hao kuungana kwa pamoja ili kuibadilisha wilaya hiyo.

Diwani wa Katumba Songwe, Fyuda Msusi, alisema miongoni mwa vipaumbele vya wilaya hiyo ni kuboresha sekta ya elimu, afya na kilimo na kwamba madiwani wamekuwa mstari kusimamia miradi inayotekelezwa.



Baadhi ya wanawake wa Jiji la Mbeya, wakitengeneza vifungashio kwa kutumia karatasi za kaki, ikiwa ni jitihada za kujikwamua kiuchumi, baada ya kupata mafunzo kutoka Shirika la ELIMISHA, juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Waomba maabara kubaini wingi dhahabu

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

WAMILIKI wa viwanda vya kuchenjua dhahabu wilayani Chunya, wameiomba serikali kuwajengea maabara ya kisasa yenye uwezo wa kubaini wingi wa dhahabu kwenye udongo kabla ya kuchenjuliwa.

Wamesema hatua hiyo itawasaidia kuepuka hasara na kutoaminiana baina yao na wachimbaji wa madini hayo.

Ombi hilo lilitolewa juzi na na baadhi ya wamiliki wa viwanda vya kuchenjua dhahabu mbele ya Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru, Luteni Josephine Mwambashi, wakati akizindua kiwanda cha kuchenjua dhahabu cha Kindai, kilichoko katika Mji Mdogo wa Makongorosi.

Mmiliki wa kiwanda hicho, Hamisi Rajabu, alisema uwapo wa maabara hiyo kutasaidia kuongeza kasi ya uchimbaji wa dhahabu na kuongeza wigo wa ajira kwa wananchi wa Chunya.

"Uwepo wa maabara hiyo utasaidia kupunguza malalamiko kwa wafanyabiashara wadogo wanaouza dhahabu kwenye vituo maalumu vya kuuzia bidhaa hizo," alisema Rajabu.

Luteni Mwambashi aliwataka wamiliki wa viwanda hivyo kutokatishwa tamaa na vikwazo hivyo huku akiwapongeza kwa kutoa ajira kwa vijana.

Alisema kiwanda hicho tayari kimeajiri vijana 21 ambao nao wamekuwa msaada kwa familia yao na kujiepusha na vitendo mbalimbali vya uhalifu vikiwamo wizi na uvutaji bangi.

Mwenge wa Uhuru umemaliza mbio zake mkoani Mbeya na tayari Mkuu wa Mkoa, Juma Homera, ameukabidhi kwa Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba.

# Waomba ushirikiano mapambano ukatili

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WADAU wa mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia katika Mkoa wa Mbeya wameomba ushirikiano kuanzia ngazi ya familia, ili kukabiliana na vitendo hivyo.

Akizungumza juzi na Nipashe, Mratibu wa Dawati la Jinsia na Watoto Mkoa wa Mbeya, Loveness Mtemi, alisema lengo la mpango huo ni kutokomeza vitendo hivyo ambavyo ni vya ubakaji, ulawiti na vipigo.

Mtemi alisema licha ya wanawake na watoto kuwa wahanga wa matukio hayo kuna tatizo la watu hao kutotoa taarifa wanapofanyiwa vitendo vya kikatili.

"Kuna tatizo kubwa ya vitendo vya ukatili wa kingono kwa wanawake na watoto mbaya zaidi hawatoi ushirikiano kwa Jeshi la Polisi wanawakumbatia watuhumiwa kutokana na mahusiano waliyonayo kwenye familia zao naomba tubadilike," alisema Mtemi.

Ofisa Ustawi wa Jamii kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya, Anna Gloria Gereta, alisema hospitali hiyo imekuwa ikipokea watoto wengi ambao wanafanyiwa vitendo vya ukatili.

Alisema miongoni mwa vitendo vinavyoripotiwa ni ulawiti kwa watoto wa kiume na wa kike na kwamba wanapohitaji ushirikiano kutoka kwa wazazi wanakosa.

Gereta alisema licha ya hospitali hiyo kupokea watoto wanaofanyiwa vitendo hivyo alidai mpango mkakati huo waliokubaliana katika kikao hicho utaleta tija kwa kuwa wataendelea kutoa elimu kwa kuwashirikisha wazazi na walezi.

Aliongeza kuwa wanaendelea na jitihada za kutoa elimu kwa wananchi ili kujenga uelewa wa namna ya kuepukana na vitendo hivyo.



## Watakiwa kutangaza fursa Bahari ya Hindi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WADAU wa jumuiya ya nchi zilizoko kwenye mwambao wa Bahari ya Hindi wametakiwa kuzitangaza fursa zilizoko nchini ili kuimarisha uwekezaji katika sekta ya uvuvi.

Hayo yalielezwa jana na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Ikulu, Mussa Haji Ali, wakati akifunga kikao cha siku tatu cha wadau wa jumuiya ya nchi zilizopo kwenye mwambao wa Bahari ya Hindi kilichofanyika Maisara Mjini Unguja.

Alisema fursa zilizopo katika Bahari ya Hindi ni nyingi ikiwamo uwekezaji katika sekta ya uvuvi wa bahari kuu ambao unaleta faida kubwa katika kukuza uchumi wa bluu nchini.

Alieleza kuwa, serikali inatambua umuhimu wa jumuiya ya nchi zilizopo kwenye mwambao wa Bahari ya Hindi hasa katika kuutangaza utalii ambao unasaidia katika kukuza uchumi wa taifa.

Alisema serikali zote mbili zinaendelea kufanya jitihada za kuimarisha matumizi bora ya bahari ikiwamo kupiga vita uvuvi haramu katika bahari ili kulinda uchumi wa bahari.

Aidha, katibu huyo alisema ziara zilizofanywa na wadau hao ya kutembelea kituo cha kutotolea vifaranga Kibweni na Mamlaka ya Bahari Kuu Fumba ziwe ni chachu ya kuibua mawazo mazuri yatakosaidia katika kufanikisha uchumi wa bluu nchini.

Naye Naibu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu, Dk. Emmanuel Sweke, alisema ipo haja ya kuwahamasisha wazawa kuwekeza katika uvuvi wa bahari kuu ili rasilimali za taifa zitumike kuwanufaisha wananchi.

Alisema kuwa wawekezaji wengi wanaokuja kuwekeza katika sekta ya uvuvi wa bahari kuu ni wageni, hivyo ipo haja ya kuwawezesha wazawa kimtaji ili kuwekeza.

Aidha, alipendekeza ujenzi wa bandari ya uvuvi nchini, ujenzi wa viwanda vya samaki, upatikanaji wa boti, na ufugaji wa samaki ufanyike nchini ili rasilimali ya bahari ilete manufaa makubwa zaidi kwa taifa na kuzalisha ajira kwa Watanzania.

Wadau wa jumuiya ya nchi zilizopo kwenye ukanda wa Bahari ya Hindi walipata fursa ya kutembelea kituo cha kutotolea vifaranga vya samaki Kibweni na Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Fumba.

# Waziri Mkuya afichua athari dawa za kulevya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MADHARA yatokanayo na dawa za kulevya yametajwa kuathiri kwa kiasi kikubwa maendeleo ya nchi katika maeneo mbalimbali.

Imeelezwa kuwa matumizi, usafirishaji na usambazaji wa dawa hizo umesababisha matokeo mabaya ya kiafya, ustawi wa jamii, uchumi na mazingira.

Hayo yalielezwa jana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Saada Mkuya, wakati akiwasilisha taarifa ya dawa za kulevya kwa mwaka 2019/2020 katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Alisema watumiaji wa dawa za kulevya wapo katika hatari ya kupata maradhi mbalimbali yakiwamo ugonjwa wa mapafu, akili, moyo, utegemezi wa dawa za kulevya, shinikizo la damu, maambukizi ya Virusi vya Ukimwi na homa ya ini B na C

Alisema matumizi ya dawa za kulevya kwa kiwango kikubwa (overdose) husababisha vifo vya ghafla hasa miongoni mwa wanaojidunga sindano.

Alieleza kuwa pia matumizi ya dawa za kulevya yanahusishwa na mfarakano wa kifamilia hasa ikiwa mmoja wao ni mtumiaji, kutengwa na jamii, mmong'onyoko wa maadili na kuongezeka kwa watoto wanaozurura mitaani.

"Usalama wa jamii pia umekuwa hatarini kwa kuwa watumiaji wengi wanajihusisha na vitendo vya uhalifu kama vile wizi, magenge ya uporaji, ubakaji na uharibifu wa mali na miundombinu," alisema.

Alisema maumbile ya visiwa kijiografia bado yanaleta ugumu katika kudhibiti uingiaji wa dawa za kulevya Zanzibar.

Aliongeza kuwa: "Kwa mujibu wa taarifa kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na Dawa za Kulevya na Uhalifu Duniani (UNODC), nchi za ukanda wa Afrika Mashariki na Kusini zinatajwa kuwa ni miongoni mwa njia za kupitishia dawa za kulevya aina ya heroini zinazotoka Afghanistani na kuelekea Asia, Mashariki ya Kati, Ulaya na Marekani."

Alisema ripoti za Kitengo cha Polisi cha Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar zimeonyesha katika kipindi cha miaka tisa iliyopita (2012-2020), jumla ya watuhumiwa 3,810 wakiwamo wanaume 3,577 na wanawake 233 wamekamatwa nchini wakijihusisha na uhalifu wa dawa za kulevya.

Alisema katika kipindi hicho jumla ya kilo 51.5 za heroini, kilo 2,946 za bangi, kilo 5.4 za valiamu na kilo 19.71 za coceni zilikamatwa.

Dk. Mkuya alieleza kuwa kabla ya mwaka 2016 idadi ya kesi zilizokamatwa ilikuwa ipo chini, wakati uuzaji na utumiaji wa dawa za kulevya ulikuwa ukifanyika wazi katika maeneo mengi.

Alisema miongoni mwa matatizo ya dawa za kulevya Zanzibar yanachochewa na sababu mbalimbali zikiwamo shindikizo rika, kuiga, malezi mabaya, binaadamu kutokuwa na uwezo wa kujikwamua na matatizo anayokabiliana nayo na kuwa na marafiki wenye tabia mbaya.



Waziri wa Fedha na Mipango Zanzibar, Jamal Kasim, akijibu swali katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani nje ya Mji wa Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Tarehe kesi ya maimamu yatajwa

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

KESI ya Jumuiya ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA) dhidi ya Mwanasheria Mkuu na Bodi ya Ushauri wa Udhibiti wa Vileo (ZLB) itaanza kusikilizwa na Jaji wa Mahakama Kuu, Abdulhakim Ameir Issa, Oktoba 13, mwaka huu.

Akizungumza juzi katika Mahakama Kuu Vuga, Jaji Abdulhakim, alisema, kesi itaanza kwa kusikiliza pingamizi zilizowasilishwa mahakamani na wanasheria wa serikali kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wakiongozwa na Ali Issa Abdalla.

"Mheshimiwa, kwa upande wetu tupo tayari kuanza kusikiliza kesi na hoja za msingi zimewasilishwa kwa wahusika kupitia wakili wao." alisema Mwanasheria Abdalla.

Hata hivyo, Wakili Omar Shehe Omar aliomba kesi iharishwe kusikilizwa kutokana na kukabiliwa na matatizo ya kiafya, lakini Mwanasheria wa Serikali alipinga maombi ya kutaka kesi kuahirishwa.

Lakini Jaji Abdulhakim alikubali maombi ya kuahirishwa kwa kesi na kuwataka mawakili wanawakilisha JUMAZA kupitia hoja za msingi za pingamizi kabla ya kuanza kusikilizwa Oktoba 13, mwaka huu.

Kwa mujibu wa hati ya kiapo ya maombi Jumuiya ya Maimamu Zanzibar wanadai Sheria Namba 9 ya Vileo ya Mwaka 2020 imevunjwa na Bodi ya Ushauri na Udhibiti wa Vileo Zanzibar.

Walisema kwa mujibu wa kifungu cha 33(1), kampuni tatu ndio zinatakiwa kupewa kibali cha kuingiza pombe Zanzibar baada ya kushinda zabuni, lakini zaidi ya kampuni nane zimepewa vibali kinyume na masharti ya sheria.

Aidha, wamedai kifungu cha 28(K) cha sheria ya vileo kimeweka masharti ya leseni ya baa kutolewa kwa mashariti baa iwe umbali wa mita 1,000 kutoka katika maeneo ya huduma za jamii kama shule, hospitali nyumba za ibada na makazi, lakini bodi ya vileo imeshindwa kusimamia masharti ya sheria.

Wakati kesi hiyo inapangwa kusikilizwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussen Ali Mwinyi ameivunja Bodi ya Ushauri na Udhibiti wa Vileo Zanzibar tangu Septemba 7, mwaka huu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MRATHI NA. 67 YA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**ANNETTE ERICA MAHIMBO**
**MWOMBAJI**
**KELVIN MICHAEL SIMKANGA**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki na Mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamiaji wa Mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu. Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 7 Mwezi wa 10, 2021.

**Imewasilishwa Dar es salaam, leo tarehe 14 Mwezi wa 9, 2021.**

NAIBU MSAJILI

116463902

## KUPOTEA KWA CHETI

Chama cha Wawekezaji Binafsi katika Elimu (TAPIE) kinatangaza kupotea kwa cheti chake cha usajili chenye namba S.A 20265. RB/449279/2021

116464002


## KUPOTEA KWA VYETI



**FRANK BILASHOBOKA** anatangaza kupotelewa na cheti che kidato cha nne chenye index namba **S0638-0105** kilichotolewa na **BUNAZI SEKONDARI** mwaka 2010. Cheti cha Chuo chenye namba **10/CBA-11/FM/14D/073** kilichotolewa na **VETA** Mbeya mwaka 2014. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **STK/RB/806/2019.**

116464202

## KUPOTEA KWA CHETI



**ROH YOHANA MVUWANGO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1584/0072** kilichotolewa na **KIWANJA HIGH SCHOOL mwaka 2019.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya polisi: **SO/RB/3140/2021.**

116464302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MBEYA**
**SHAURI LA RUFAA YA ARDHI NA. 56/2021**
**(Asilia kutoka Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilayaya Mbeya Maombi Na 203/2020)**
**DEBORA RAMADHANI NYAMIZI……………………………MRUFANI**
**DHIDI YA**

- **EMMANUEL JORAM KASEKWA**
- **FINCA MOCROFINANCELTD…WARUFANIWA**
- **PETER MUHEZYA MBOYA**

**Kwa: EMMANUEL JORAM KASEKWA**

**POPOTE MLIPO.**
**KUITWA SHAURINI MJIBU RIFAA NA. 1**

Unataarifiwa vna Mahakam hii kuhudhuria hapa mahakama kuu kanda ya Mbeya tarehe 29/09/2021 siku ya jumatano saa 3:00 asubuhi, ambapo sauri limepangwa kusikilizwa.

ELEWA KWAMBA ukikosa kufika siku hiyo shauri litasikilizwa bila wewwe kuwepo na uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri a mahakama leo hii tarehe 14 Mwezi September , Mwaka 2021

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MBEYA**

116464402

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **MICHAEL MIRAJI CHONYA** amepoteza kadi ya gari namba **T 305 DUE** aina ya **Mark X**. Taarifa za upotevu zimefunguliwa kituo cha Polisi Bukoba kwa jalada namba **KAG/BUK/RB/448521/2021** atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi

116464602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MBEYA**
**SHAURI LA RUFAA YA ARDHI NAMBA.33/2021**
**[Asilia kutoka Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Mbeya Maombi Na 37/2018]**
**HAMIS MLOWEA ……………………………MRUFANI**
**DHIDI YA**
**1: KAPUNGA VILLAGE COUNCIL**
**2: SANGALALI MASHISHANGA ……………..WARUFANIWA**
**Kwa: SANGALALI MASHISHANGA**

**POPOTE MLIPO.**

**KUITWA SHAURINI MJIBU RUFAA NA 2.**
Unataarifiwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakama Kuu Kanda ya **Mbeya tarehe 06/10/2021** siku ya **Jumatano saa 3;00 asubuhi**, ambapo shauri limepangwa kusikilizwa.
**ELEWA KWAMBA** ukikosa kufika siku hiyo shauri litasikilizwa bila wewe kuwepo na uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo hii tarehe 13 mwezi Septemba,Mwaka 2021.

……………………………………………………
**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MBEYA**

116464702

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.107 OF 2021**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE FLORA MTANINGU SIMON**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY ELLYNEEMA SUDA MWASALANGA.**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the **13 Day of OCTOBER 2021.**

**Dated at Dodoma this 9TH day of September 2021.**

MAGISTRATE

116464902

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **FREDINAND PASCHAL SHIRIMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MITSUBISHI CANTER** yenye namba za usajiri **T 991 DSG.** **Chassis namba FE315BD445323.** **Engine namba 4D445323** **Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.** **Taarifa Polisi: TAN/RB/449337/2021**

116465502

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **FREDINAND PASCHAL SHIRIMA** wa **Box 276** korogwe anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajiri **T 991 DSG.** Chassis namba **FE315BD445323**. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. **Taarifa Polisi: TAN/RB/449343/2021**

116465802

**FreedomPath (T) LTD**
Debt Collectors, Auctioneers, & General Brokers

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**KWA NIABA YA VISIONARY WOMEN SACCOS LTD TUTAUZA KIWANJA TAJWA KWA MNADA WA HADHARA,**
**MAHALI:**
Kihonda, Kilimanjaro-Yespa, Manispaa ya Morogoro.
**MAELEZO:**
Kiwanja chenye hati miliki Na. 97881, Block '5", Plot#: 07, 1629sqm.

| JINA LA MDAIWA | TAREHE YA MNADA |
|---|---|
| HELLEN MOLLEL OLENGAILUVA | 01/10/2021 Ijumaa saa 5:00 asubuhi |

**MASHARTI YA MNADA**
1. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
2. Malipo salia ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14).
3. Gharama za ukaguzi na kubadili hati ni za mnunuzi

116465202

**Wasiliana nasi kupitia Namba 0754711284|0784670148**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax:+255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
,Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA

## TANGAZO

KAMPUNI YA **PMM ESTATES (2001) LTD** ITASAFIRISHA MIZIGO YENYE VIPIMO VIKUBWA KUTOKA BANDARI YA DAR ES SALAAM KWENDA **MANTRAC - DAR ES SALAAM** KWA KUTUMIA GARI ZENYE NAMBA ZA USAJILI: T**274DQV/T472CVG NA T281DQV/T473CVG.**

**VIPIMO NI KAMA IFUATAVYO:**

| | |
|---|---|
| UREFU MITA | 18, |
| UPANA MITA | 3.24, |
| KIMO MITA | 4.8. |

SAFARI IMEPANGWA KUANZA **TAREHE 17.09.2021.** NJIA ZITAKAZOTUMIKA NI BARABARA YA MANDERA NA NYERERE. GARI ZITASAFIRI MUDA WA MCHANA TU KUANZIA **SAA 12:30 ASUBUHI MPAKA 12:00 JIONI.**

**TUNAOMBA RADHI KWA USUMBUFU UTAKAOJITOKEZA**

116465202

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **IRENE FERDANARD SHIRIMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **MITSUBISHI CANTER** yenye namba za usajiri **T 314 DMQ.** Chassis namba **FE518BD420967.** Engine namba 4D351AZF0306 Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. **Taarifa Polisi: TAN/RB/449343/2021**

116465902

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **IRENE FERDANARD SHIRIMA** wa **Box 276** Korogwe anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajiri **T 314 DMQ.** **Chassis namba FE518BD420967.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. **Taarifa Polisi: TAN/RB/449343/2021**

116465602

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **HAFIDH TAHIR HAFIDH** anatangaza kupotelewa na kadi pikipiki yenye namba za usajiri **MC 652 BHH.** Chassis namba **LJEPCJL09GA002030.** **Engine** namba **157FMIG3A80524.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa Polisi: **TAN/RB/442333/2021**

116460202

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BURTON BATAZAL RUTTA** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 969 DDD** TOYOTA SIENTA. **CHASSIS NAMBA NCP810020370.** ENGINE **NAMBA IZDEAA0370.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. **TAARIFA YA POLISI: MKB/TR/RB/179/2021.**

116466002

**MATANGAZO MCHANGANYIKO**

PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA ENTEPRISES FINANCE LIMITED (EFL).
KWA MAWASILIANO ZAIDI
**TUPIGIE:0677 111 333**
**AU 0758 112 332**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe

116460302

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



Katibu wa CCM Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shuka, akisaidia kupaka rangi wakati alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa Shule ya Sekondari ya wavulana Nachingwea, mkoani Lindi jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri awatoa hofu wamiliki viwanja kuhusu uhakiki ardhi

**Na Munir Shemweta,** BUKOMBE

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewatoa hofu wamiliki wa ardhi kuhusu uhakiki unaoendelea huku akiwataka kujitokeza katika kazi ya uhakiki inayoendelea katika ofisi zote za ardhi nchini.

Kwa mujibu wa Dkt Mabula, kumekuwa na sintofahamu kuhusiana na uhakiki ambao baadhi ya watu wanasita na kufikiri serikali inataka kuwanyang'anya viwanja. alisisitiza kuwa, lengo ni kutaka kuwatambua wamiliki kwa majina yao na kubainisha kwamba kama kuna majina ya watoto basi yatatenganishwa vya kwao na vya watoto

Akizungumza na viongozi pamoja na watumishi wa sekta ya ardhi katika Wilaya ya Bukombe mkoani Geita juzi, Mabula alisema hatua ya kufanya uhakiki itaisaidia wizara na serikali kupata kumbukumbu nzuri za Watanzania wanaomiliki ardhi na kusisitiza kuwa hakuna ukomo kwenye umiliki na mtu mmoja anaweza kumiliki hata zaidi ya viwanja 20.

Alisema uamuzi wa wizara yake kufanya uhakiki wa wamiliki wa ardhi ni kutaka kuwatambua kwa majina yanayosomeka kwenye vitambulisho vya NIDA.

''Tunachotaka ni kukutambua kama wewe ni mmiliki wa kiwanja kilichopo Bukombe au Sumbawanga kwa majina yale yale yanayosomeka katika kitambulisho cha NIDA,'' alisema.

''Tunachotaka ni kuondoa wamiliki bandia ambao hata ukiwatafuta huwapati kwa kuwa jina aliloandika siyo la kwake na kama kuna majina ya watoto basi yatenganishwe na ya kwako,'' alisema.

Pia alisema kuwa uhakiki unaoendelea utasaidia pia kwenye masuala ya mirathi hasa pale mmiliki atakapofariki dunia huku akiwa hakutumia majina yake kwenye umiliki wa viwanja vyake na kuongeza kuwa ikitokea mmiliki amefarikia dunia basi familia yake ijue rasilimali zake.

Mkuu wa Wilaya ya Bukombe, Said Nkumba, alimshukuru Naibu Waziri kwa kuitembelea wilaya hiyo na kukutana na viongozi pamoja na watumishi wa sekta ya ardhi.

Nkumba alisema ujio wake utasaidia wilaya yake kujipanga katika masuala ya ardhi hasa kwenye matumizi bora ya ardhi.

Nkumba pia aliunga mkono wazo la Naibu Waziri kutaka Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe kuangalia namna ya kuwakopesha viwanja watumishi wa serikali walioko kwenye wilaya hiyo ili wajikwamua katika masuala ya makazi.

''Kama huwezi kukopa basi hata kukopa kiwanja? Nafikiri suala la kukopa viwanja ni jambo jema na ni vizuri tukaanza na watumishi kwa kuwa unalipa kidogo kidogo na huwezi kujua unaweza kukaa hapa Bukombe mpaka unastaafu na sisi tunaona ni jambo jema,'' alisema Mkumba.

# Jela maisha kudhalilisha mtoto wa miaka 4

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MAHAKAMA ya Wilaya ya Babati mkoani Manyara imemhukumu mkazi wa Magugu, Edward Shedrack, kutumikia kifungo cha maisha jela baada ya kukutwa na hatia ya kumlawiti mtoto wa miaka minne.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Victor Kimario.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Kimario alisema mshtakiwa alitenda kosa hilo Agosti 3, mwaka huu.

Hakimu Kimario alisema mshtakiwa alikiuka Kifungu cha 154(1)(a) na (2) cha Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

Katika shauri hilo namba 72 la mwaka huu, Hakimu Kimario alisema kuwa baada ya kusikiliza ushahidi uliotolewa mahakamani huko na mtoto pamoja na mashahidi wengine, ameridhika nao.

"Mtoto alitoa ushahidi kwa lugha inayoeleweka na ushahidi wake hautikisiki, alisema alimfanyia kitu kibaya," alisema Kimario.

Hakimu alimpa nafasi ya kujitetea mshtakiwa ambaye aliiomba mahakama kumpunguzia adhabu kwa kuwa baba yake ni mlemavu wa mkono na anamtegemea kwa kuwa mama yake amefariki dunia.

Hakimu Kimario baada ya kusikiliza utetezi wa mshtakiwa huyo, alisema licha ya kuwa hilo ni kosa la kwanza kwa mshtakiwa, mahakama inamtia hatiani na inampa adhabu hiyo.

Alisema kwa kutenda kosa hilo, sheria inasema mtu akimlawiti mtoto chini ya miaka 10 adhabu yake ni kifungo cha maisha gerezani.

Awali Wakili wa Serikali, Grace Mgaya, alidai licha ya kwamba mshtakiwa hana rekodi ya kutenda makosa, mahakama inapaswa kutoa adhabu kali ili iwe fundisho kwa watu wengine.

Mgaya alidai kuwa mshtakiwa huyo apewe adhabu kali kwa kuwa kitendo alichomfanyia mtoto huyo kitamwathiri kisaikolojia.

# Serikali yatoa bil. 3/- kuwalipa wauguzi

**Na Maulid Mmbaga**

SERIKALI nchini imeidhinisha Sh. bilioni tatu kwa ajili ya malipo kwa watumishi wa sekta ya afya waliotoa ushirikiano katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alipokuwa akizungumza na watumishi wa afya katika Hospitali ya Rufani ya Tumbi mkoani Pwani, alipofanya ziara ya kikazi ya kukagua utoaji huduma katika hospitali hiyo.

Alisema watumishi wa afya walizungumzia suala la fedha zao wakati wanapambana na UVIKO-19, na alithibitisha kuwa tayari Rais Samia Suluhu Hassan ameshazitoa kwa ajili ya waliokuwa wanajitoa kwa kufanya kazi mbalimbali katika kuwahudumia wagonjwa waliopata ugonjwa huo.

"Katika kulikamilisha hilo ndani ya muda wa wiki mbili watumishi wote halali wanaopaswa kulipwa fedha hizo watakuwa wameshapata malipo yao," alisema Mollel.

Aliongeza kuwa serikali imetenga kiasi cha Sh. bilioni 187 kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza chanjo za magonjwa mbalimbali ikiwamo ugonjwa wa corona.

Katika juhudi zinazoendelea kufanywa na serikali katika upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi, alibainisha kuwa Rais Samia ametoa Sh bilioni 149.7 kwa ajili ya kugharamia watu maskini wasiojiweza kupata huduma za matibabu katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

Pia, wanatarajia watu wote nchini watakuwa na bima ya afya kwa kuwahusisha Watanzania wanaoweza kujilipia na wale wasioweza kwa kuwa tayari serikali imeshawalipia.

"Kwa muda wa miaka nane sasa mchakato wa kuwasilisha muswada wa bima ya afya kwa wote umekuwa ukikabiliwa na changamoto mbalimbali na hivyo sasa serikali imejipanga kuwasilisha kuwa sheria katika mkutano wa Bunge wa mwezi Novemba," alisema Mollel.


**STEAM**

Generation Recoveries Ltd

2nd Floor, Shamo Tower, Plot No 246/247 Block D Mbezi Beach New Bagamoyo Road,
P. O. Box 80607 Dsm, Tz
Tel/ Fax: +255 222 618611/ Mob: +255 715 91 74 51, Email: steam@steamtz.com website: steamtz.com

## NOTISI /TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA MICROFINANCE BANK**; Tunatoa notisi ya siku 14 kwa mdaiwa kulipa deni la Benk, baada ya hapo tutauza Kwa mnada wahadhara dhamana/mali ya mdaiwa alieshindwa kurejesha mkopo wa Bank hiyo.

**Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo Kama ifuatavyo:**

216466102

| Na | JINA LA MDAIWA | JINA LA MWENYE DHAMANA | DHAMANA | TAREHE/MUDA | BENKI. |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | DOREEN DANIEL MAGESA | DOREEN DANIEL MAGESA | GARI NO. T493 BKQ TOYOTA CARINA, MBEZI BEACH. | KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI | MWANGA HAKIKA BANK |

**MASHARTI YA MNADA**

i. Mali Dhamana itauzwa kama ilivyo.
ii. Mshindi atatakiwa kulipa malipo ya awali ya (25%) ya kiasi alichoshinda na salio la 75% kulipwa ndani ya siku 14 tokea siku yamnada.
iii. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti na mbili hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.
iv. mnada. Malipo yote yanayohusu nyumba/viwanja au gari ni lazima yafanyike kwenye akaunti maalum ya makusanyo itakayotolewa na Afisa wa benki.
v. Gharama zote za kubadilisha taarifa za nyaraka za umiliki au kumuondoa mkazi katika nyumba zitagharamiwa na mnunuzi.
vi. Kwa maelezo Zaidi wasiliana na Dalali kwa mawasiliano yaliyotolewa hapo juu.

MECHI KALI
HOME
AWAY
NEWCASTLE
3.01 | 3.57 | 2.26
LEEDS
1 WEKA PESA.
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4 - WEKA PESA.
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND
2 WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 499



# LAPORTA AWATAKA BARCA KUTULIA, KUVUMILIA

**BARCELONA,** Hispania

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta ametaka utulivu na uvumilivu kutoka kwa mashabiki wa timu hiyo wakati yeye akijaribu "kutatua" matatizo yanayoikabili klabu hiyo ya Katalunya yanayotokana ukata wa fedha.

Matatizo ya kifedha pamoja na sheria mpya ya matumizi ya mishahara kwenye Ligi Kuu ya Hispania, yakaifanya Barca kumpoteza Lionel Messi aliyejiunga na Paris Saint-Germain kwa uhamisho huru.

Antoine Griezmann, pia amepelekwa kwa mkopo kwa wapinzani wao, Atletico Madrid huku kukiwa na kipengele cha kununuliwa moja kwa moja.

Barca ilikumbana na kipigo cha mabao 3-0, kutoka kwa Bayern Munich kwenye mchezo wa kwanza wa kundi wa Ligi ya mabingwa Ulaya, Jumanne na kuzidisha hali mbaya kwenye viunga vya Camp Nou.

Huku mashabiki sasa wakiwa wameanza kupaza sauti kuhusu hali ilivyo kwa miamba hao wa LaLiga, Laporta ametoa taarifa kupitia video aliyoiweka kwenye mitandao ya kijamii jana kuhusiana na hali hiyo.


"Jamani. Nimekatishwa tamaa na hali jinsi ilivyo kwa sasa kama ambavyo nyinyi mnaiona," alisema.

"Nahitaji kuwaambia nini kinachotokea. Hii ni hali ambayo tuliitarajia kwani ipo nje ya uwezo wetu kwa sasa.

"Nawaomba wote kuwa watulivu na kwamba endeleni kutoka sapoti kwa timu yenu. Nawaomba muendelee kutuamini sisi, na watu wote ambao wanahusika na uongozi kwa klabu hii.

"Tunahitaji kuaminiana kila wakati. Bila shaka yoyote tutapata ufumbuzi wa tatizo hili na hali itarudi kuwa kawaida."

# SIMEONE: GRIEZMANN ATARUDI KWENYE UBORA



**MADRID, Hispania**

DIEGO Simeone ana matumaini Antoine Griezmann haraka atajibu shutuma anazopewa na mashabiki wa Atletico Madrid kwa vitendo, baada ya kutoka suluhu na Porto kwenye mchezo wa Ligi ya mabingwa Ulaya, Jumatano.

Atletico walishindwa kupata ushindi kwenye mchezo wao wa kwanza wa ufunguzi wa Ligi ya mabingwa Ulaya, kwa mara ya tatu mfululizo.

Griezmann aliingizwa kipindi cha pili wakati kocha huyo akitafuta ushindi kwenye mchezo huo, lakini hakuweza kutoa msaada wowote na alishindwa kugusa mpira kwenye eneo la box la Porto.

Mashabiki wa klabu hiyo wamekuwa wakimzomea fowadi huyo wa Ufaransa, ambaye kuondoka kwake kwenda kule Camp Nou hakukuwafurahisha na sasa wanamuona kama msaliti, ambaye hana msaada kwa timu.

Lakini Simeone amemtetea Griezmann, ambaye mabao yake 21 kwenye Ligi ya mabingwa Ulaya na Atletico yanafanya kuwa mbele kwa mabao tisa zaidi ya mchezaji yeyote wa kikosi hicho, anaamini ataimarika na kuwajibu mashabiki kwa vitendo.

"Hebu tutarajie (Griezmann) atakuwa bora zaidi, anaweza kujibu shutuma kwa kazi nzuri," alisema Simeone akiiambia Movistar.

"Anakabiliwa na changamoto kubwa mbele yake na hasa kutokana na matokeo ya timu pamoja na yeye kushindwa kufunga."

## HABARI MICHEZO



# GUARDIOLA AMWAGA SIFA KIBAO KWA GREALISH

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amemsifia mchezaji aliyesajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi klabuni hapo, Jack Grealish bada ya kuwa na usiku wa kukumbukwa kwenye mchezo wake wa kwanza wa Ligi ya mabingwa Ulaya, wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 6-3, dhidi ya RB Leipzig.

Grealish - ambaye aliwasili hapo kutoka Aston Villa kwa ada iliyoripotiwa kuwa ni pauni milioni 100, wakati wa dirisha la kipindi cha majira ya joto - alifunga kwenye ushindi huo wa City, Jumatano.


Mchezaji huyo wa kimataifa wa England alicheza vizuri na Nathan Ake aliyeifungia City bao la uongozi dakika ya 16, kabla yeye kufunga lake kipindi cha pili.

Grealish amekuwa mchezaji wa kwanza wa Uingereza kucheza mchezo wa kwanza wa Ligi ya mabingwa Ulaya, akifunga na kutoa asisti, tangu nyota wa zamani wa Manchester United, Wayne Rooney alipofanya hivyo, dhidi ya Fenerbahce, Septemba 2004.

"Matumaini yetu yatakuwa mengi zaidi ya hili moja," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari kumzungumzia Grealish mara baada ya mchezo huo.

"Nina hisia kwamba, kila siku atacheza vizuri na kuwa bora na nina uhakika mkubwa atakuwa bora zaidi kwa siku za usoni.

"Mchango wake ulikuwa mkubwa sana na mzuri. Nimefurahishwa na kuhamasika na kiwango chake, kwenye mchezo wake wa kwanza wa Ligi ya mabingwa Ulaya."



# ANCELOTTI ATOA SABABU KUTOMCHEZESHA HAZARD

**MADRID, Hispania**

EDEN Hazard hakuwa uwanjani wakati Real Madrid wakishinda, dhidi ya Inter Milan kwenye mchezo wa kwanza wa makundi wa Ligi ya mabingwa Ulaya na kocha, Carlo Ancelotti ameelezea kwanini alimuazisha Rodrygo badala ya winga huyo wa Ubelgiji.

Madrid walilazimika kusubiri hadi dakika ya mwisho kwenye mchezo huo, ili kuweza kupata ushindi, huku golikipa, Thibaut Courtois akifanya kazi nzuri ya kuokoa hatari za Edin Dzeko na Lautaro Martinez kwenye mchezo huo wa kundi D.

Rodrygo aliingia kuchukua nafasi ya Lucas Vazquez dakika ya 65, wakati Los Blancos wakionekana kubanwa kwa dakika nyingi za mchezo huo, kabla ya kupata bao hilo la ushindi.

Alipoulizwa kwanini Hazard, ambaye alicheza kwa dakika 66 katika ushindi wa 5-2, kwenye mchezo wa LaLiga dhidi ya Celta Vigo mwishoni mwa wiki, hakuchezeshwa dhidi ya Inter, Ancelotti alijibu: "Nilifikiria kumuingiza kipindi cha pili, lakini Inter walipafunga katikati ya dimba vizuri.

"Nilitaka kuufungua mchezo kwa kutumia winga, ndio maana nikaamua kumuingiza Rodrygo."

Rodrygo bado hajaanza mchezo wowote chini ya Ancelotti, lakini sasa amefunga kwenye mechi mbili kati ya tatu alizocheza kwenye Ligi ya mabingwa, dhidi ya Inter - zote, mara zote akifunga bao la ushindi.

"Nilimuambia sio kufikiria ni dakika ngapi amecheza, lakini sasa anacheza kila akipata nafasi," alisema Ancelotti akiwaambia waandishi wa habari."


,059,740

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 18.9.21 | 17:00 | Derby vs Stoke City | 3.00 | 3.15 | 2.36 |
| 2. 18.9.21 | 17:00 | Millwall vs Coventry | 2.47 | 3.17 | 2.82 |
| 3. 18.9.21 | 17:00 | Cardiff vs Bournemouth | 2.86 | 3.31 | 2.36 |
| 4. 18.9.21 | 17:00 | Barnsley vs Blackburn | 2.77 | 3.16 | 2.52 |
| 5. 18.9.21 | 18:00 | Lens vs Lille | 2.49 | 3.29 | 2.79 |
| 6. 18.9.21 | 19:30 | Aston Villa vs Everton | 2.46 | 3.27 | 2.92 |
| 7. 18.9.21 | 19:30 | Elche vs Levante | 2.67 | 3.13 | 2.77 |
| 8. 18.9.21 | 22:00 | Alaves vs Osasuna | 3.02 | 3.12 | 2.48 |
| 9. 19.9.21 | 13:30 | Empoli vs Sampdoria | 2.52 | 3.63 | 2.62 |
| 10.19.9.21 | 14:00 | Nice vs Monaco | 2.73 | 3.38 | 2.48 |
| 11. 19.9.21 | 16:00 | Brighton vs Leicester | 2.83 | 3.19 | 2.58 |
| 12. 19.9.21 | 17:15 | Real Sociedad vs Sevilla | 2.56 | 3.17 | 2.86 |
| 13. 19.9.21 | 21:45 | Juventus vs AC Milan | 2.36 | 3.32 | 3.03 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 17 - SEPTEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 5736 | Tsarsko Selo vs Lokomotiv Plovdiv | 4.26 | 3.34 | 1.78 |
| 17:00 | 3398 | Novi Pazar vs Radnicki Nis | 2.51 | 3.34 | 2.51 |
| 18:00 | 3579 | Spartak Trnava vs SKF Sered | 1.41 | 4.45 | 6.19 |
| 18:15 | 4902 | Arda Kurdzhali vs Pirin Blagoevgrad | 1.78 | 3.35 | 4.27 |
| 19:00 | 2441 | Ionikos Nikea FC vs Aris Salonica | 4.26 | 3.37 | 1.84 |
| 19:00 | 3499 | Como vs Frosinone | 3.16 | 3.01 | 2.34 |
| 19:00 | 5163 | Zaglebie Lubin vs Nieciecza KS | 1.98 | 3.19 | 3.62 |
| 19:10 | 3653 | Wacker Innsbruck vs FC Liefering | 2.09 | 3.68 | 2.90 |
| 19:30 | 2360 | Schalke 04 vs Karlsruher SC | 2.00 | 3.46 | 3.51 |
| 19:30 | 2803 | Nurnberg vs Hansa | 1.75 | 3.55 | 4.54 |
| 19:30 | 3023 | SV Horn vs Kapfenberg | 1.95 | 3.53 | 3.34 |
| 19:30 | 3805 | SV Lafnitz vs SKN St Polten | 2.23 | 3.43 | 2.81 |
| 19:30 | 4307 | Amstetten vs Blau Weiss Linz | 3.20 | 3.54 | 2.00 |
| 19:30 | 4961 | FC Juniors OO vs Austria Vienna II | 2.71 | 3.48 | 2.28 |
| 19:30 | 5530 | Desna Chernigov vs Rukh Vinnyky | 1.79 | 3.78 | 3.68 |
| 20:00 | 1021 | Torpedo Zhodino vs Energetik Bgu Minsk | 1.82 | 3.48 | 3.87 |
| 20:00 | 1274 | Laval vs Le Mans | 2.44 | 2.89 | 3.04 |
| 20:00 | 1335 | Covilha vs Penafiel | 2.53 | 2.97 | 2.83 |
| 20:00 | 1655 | Chambly vs Bastia Borgo | 1.85 | 3.27 | 4.20 |
| 20:00 | 1928 | Radnik Surduluca vs Vojvodina | 2.71 | 3.34 | 2.34 |
| 20:00 | 2043 | Bourg Peronnas vs Chateauroux | 2.17 | 3.02 | 3.42 |
| 20:00 | 2217 | Aalborg vs Odense | 2.01 | 3.49 | 3.44 |
| 20:00 | 2574 | Sedan vs Creteil | 1.82 | 3.31 | 4.28 |
| 20:00 | 2743 | Red Star vs Villefranche Sur Saone | 2.49 | 2.98 | 2.88 |
| 20:00 | 3008 | Metalac vs Kolubara | 1.78 | 3.43 | 4.15 |
| 20:00 | 3517 | Orleans vs Annecy FC | 2.33 | 2.84 | 3.28 |
| 20:00 | 4164 | Yeni Malatyaspor vs Fatih Karagumruk | 2.62 | 3.36 | 2.52 |
| 20:00 | 4410 | Altay vs Goeztepe | 2.27 | 3.31 | 3.01 |
| 20:00 | 5111 | Boulogne vs Cholet | 1.88 | 3.13 | 4.30 |
| 20:00 | 5413 | Lyngby vs HB Koge | 1.46 | 4.46 | 5.43 |
| 20:00 | 5472 | Sete 34 FC vs Saint Brieuc | 2.55 | 2.94 | 2.84 |
| 20:30 | 2242 | Botev Plovdiv vs Beroe | 1.77 | 3.68 | 3.87 |
| 21:00 | 1239 | Hrvatski Dragovoljac vs HNK Rijeka | 8.32 | 5.22 | 1.28 |
| 21:00 | 3656 | Sparta Rotterdam vs NEC Nijmegen | 1.94 | 3.40 | 3.75 |
| 21:00 | 4251 | Rapid Bucuresti vs Gaz Metan Medias | 1.68 | 3.48 | 5.10 |
| 21:30 | 1211 | Lech Poznan vs Wisla Krakow | 1.48 | 4.16 | 5.61 |
| 21:30 | 4486 | Hertha BSC vs Greuther Furth | 1.70 | 3.88 | 4.57 |
| 21:30 | 4931 | Brescia vs Crotone | 1.78 | 3.61 | 4.25 |
| 21:45 | 1002 | Sassuolo vs Torino | 1.91 | 3.72 | 3.82 |
| 21:45 | 1059 | Newtown AFC vs Aberystwyth Town | 1.94 | 3.68 | 3.25 |
| 21:45 | 1797 | UCD Dublin vs Waterford Utd | 2.81 | 3.25 | 2.32 |
| 21:45 | 2407 | Cercle Brugge vs Eupen | 2.50 | 3.44 | 2.60 |
| 21:45 | 3634 | Bohemians FC vs Maynooth University Town FC | 1.06 | 9.07 | 23.17 |
| 21:45 | 3810 | St Patricks vs Wexford Youths | 1.10 | 7.73 | 17.39 |
| 22:00 | 1977 | Celta Vigo vs Cadiz CF | 1.55 | 4.02 | 6.23 |
| 22:00 | 2416 | Finn Harps vs Dundalk FC | 2.86 | 3.01 | 2.42 |
| 22:00 | 4382 | Alcorcon vs Almeria | 3.63 | 3.04 | 2.12 |
| 22:00 | 5586 | Newcastle vs Leeds | 3.01 | 3.57 | 2.26 |
| 22:00 | 5672 | Strasbourg vs Metz | 1.81 | 3.52 | 4.36 |
| 22:15 | 1559 | Portimonense vs Santa Clara | 2.51 | 2.91 | 3.00 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# OWEN ASEMA PSG NI DHAIFU IKIWA NA MESSI

●●●Ni baada ya sare Uefa, Rio Ferdinand ampinga adai watakuwa bora sana kwa sababu...

**LONDON, ENGLAND**

MICHAEL Owen amedai kwamba, timu ya Paris Saint-Germain imekuwa dhaifu kwa Lionel Messi kujiunga na klabu hiyo, baada ya raia huyo wa Argentina kushindwa kufunga kwenye mchezo wake wa kwanza kuanza kwa kikosi hicho cha Ufaransa.

Messi alianza kwenye mchezo wa kwanza wa makundi wa PSG, kwenye Ligi ya mabingwa Ulaya Jumatano, dhidi ya Club Bruges, akiwa pamoja na Kylian Mbappe na Neymar, lakini hakuna yeyote kati yao aliyefunga katika sare ya 1-1.

Fowadi hao watatu mbele, ambao walitajwa kwa jina la 'MNM' na vyombo vya habari vya Ufaransa hivi karibuni, ni moja kati ya upatina unaovutia zaidi kwenye soka kwa sasa, lakini nyota wa zamani wa Liverpool na England, Owen amedai kuwa hilo halitoshi kuifanya PSG, kuwa na nafasi kubwa ya kushinda Ligi ya mabingwa Ulaya.

Owen ameiambia BT Sport: "Kwa kuiangalia timu ya PSG na fowadi wale, wote ni wachezaji wa kiwango cha juu sana kwa sasa.

"Lakini wakiwa watatu pamoja wanakuwa dhaifu zaidi kwa mtazamo wangu na sielewi kwanini wao ni moja ya timu inayopewa nafasi kubwa kushinda Ligi ya mabingwa Ulaya.

"Nafikiri timu za Uingereza (Chelsea, Liverpool, Manchester City na Manchester United) ziko mbali zaidi kwa ubora."

Lakini, Rio Ferdinand, ambaye alicheza na Owen pale Manchester United wakati wa siku zake za mwisho za uchezaji, haungi mkono kauli ya straika huyo wa zamani, akidai kwamba PSG wanawachezaji nyumba ya Messi, Mbappe na Neymar wanaoweza kuwafungua mafowadi hao watatu.

"Sijui," alisema Ferdinand akimjibu Owen wakiwa kwenye uchambuzi mara baada ya mchezo huo.

"Kama ukiwaangalia waliopo nyuma yao unapata mchanganyiko mzuri zaidi kwa uwapo wa (Marco) Verratti, (Idrissa) Gueye, (Gini) Wijnaldum. "Unapata miguu mizuri, kuna watu wanaoweza kusafirisha mipira sehemu yoyote na kuleta madhara makubwa.

"Ndio, wanatakiwa kufanyia kazi mambo madogo kwa kiasi fulani, lakini naamini kwa uwezo wa Neymar, Mbappe na Messi ni suala la muda tu."

## ZISIKUPITE

### LIVERPOOL YAMUWANIA LEWANDOWSKI

LIVERPOOL imejitokeza kama mojawapo ya klabu, ambazo zinamsaka mshambuliaji wa Poland na Bayern Munich, Robert Lewandowski mwenye umri wa miaka 33, ambaye anatarajiwa kuondoka kule Munich msimu ujao. **(Fichajes)**

### FERNANDES NA MKATABA MPYA

MANCHESTER United wamekuwa na mazungumzo mazuri na kiungo wa kati wa Ureno, Bruno Fernandes tangu Julai. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 anataka kusalia Old Trafford na mkataba wake unachukuliwa kwa umuhimu mkubwa pamoja na kiungo wa kati, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 28. **(Fabrizio Romano via Twitter)**

### MAN YAACHANA NA KOULIBALY

MANCHESTER United ilitaka kufanya mazungumzo ya makubaliano na Napoli, ili kumsajili nahodha wa Senegal, Kalidou Koulibaly mwenye umri wa miaka 30 msimu ujao, lakini hawakuwa tayari kukubali thamani ya mchezaji huyo kama inavyodaiwa na klabu hiyo ya Serie A ya pauni milioni 34 kumnunua beki huyo wa kati. **(Corriere dello Sport via Express)**

### ADEYEMI ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL ipo katika nafasi nzuri kuwasilisha ombi lao Januari, ili kumsajili mshambuliaji wa Ujerumani, Karim Adeyemi mwenye umri wa miaka 19, kutoka klabu ya Austria ya Red Bull Salzburg. **(Mundo Deportivo)**

### RUDIGER KUUZWA

MLINZI wa Chelsea, Antonio Rudiger huenda akauzwa, ili kufadhili ununuzi wa beki wa Sevilla, Jules Kounde. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 raia wa Ujerumani, ananyatiwa na klabu za PSG na Real Madrid, lakini ameonekana kuwa beki muhimu kwa kocha, Thomas Tuchel. **(Football 365)**

### BARCA ILIMTAKA RODRIGO

BARCELONA ilimnyatia mshambuliaji wa Leeds United, Rodrigo mwenye umri wa miaka 30 katika siku ya mwisho ya dirisha la uhamisho msimu huu wa majira ya joto, lakini klabu hiyo ya ligi Kuu ya England ikakataa ofa hiyo kwa raia huyo wa Hispania. **(The Athletic)**

### MARTINEZ KUONGEZA MKATABA

MSHAMBULIAJI wa Inter Milan, Lautaro Martinez ameripotiwa kukaribia kutia saini mkataba mpya na klabu hiyo ya Serie A, hiyo inamaana kwamba, Arsenal na Tottenham Hotspur zitalazimika kutumia kitita kikubwa cha fedha iwapo zitaamua kuimarisha nia yao ya kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24. **(Gazzetta dello Sport)**

### WILSHERE AKATAA OFA

NYOTA wa zamani wa Arsenal, Jack Wilshere hataki makubaliano ya kulipwa kwa mechi atakazoshiriki katika uwanja wa Emirates, baada ya kocha, Mikel Arteta kumruhusu kushiriki mazoezi kwenye uwanja wa timu hiyo. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 ameichezea England mara 34, lakini amekosa klabu tangu alipoondoka Bournemouth mapema mwaka huu. **(Metro)**

### PHILLIPS APEWA OFA

LEEDS United imefungua mazungumzo na Kalvin Phillips juu ya mkataba mpya kwa kiungo huyo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 25. **(Football Insider)**

### GOLDSON AWANIWA

KLABU ya West Ham wanapambana kutaka kumsajili mlinzi wa kati wa England kutoka Rangers, Connor Goldson mwenye umri wa miaka 28, ambaye mkataba wake unamalizika kipindi cha majira ya joto yajayo. **(Football Insider)**

## Abbas: Tamasha la wanawake lilete mageuzi

Na Saada Akida

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo, Dk. Hassan Abbas amesema kupitia Michezo ya Wanawake (Tanzanite Women Festival) ilete mageuzi na kusaidia Serikali kupata mwanga wa wapi waanzie katika kuhakikisha kusaidia michezo.

Kauli hiyo imetolewa jana katika uzinduzi wa tamasha hilo kubwa kuinua wanawake kwenye sekta ya michezo, kwa ujumla ambalo litazinduliwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Samia Suluhu Hassan na kuendelea kufanyika kila mwaka.

Akizungumza katika tamasha hilo, Dk Hassan alisema wanawake wanatakiwa kuamka na kuwakumbusha wanaweza kupata fursa ya kuiwakilisha nchi kimataifa na kusema anaamini kufanyika kwa kongamano kutatoa mwongozo wa nini kifanyike kwenye kumuinua mwanamke kimichezo.

Alisema, wanawake wa Tanzania wana thamani kubwa na wanafanya vizuri katika sekta ya michezo, lakini hawapewi kipaumbele kama ilivyokuwa kwa wanaume katika michezo.

"Serikali ya awamu ya Sita ya mama Samia Suluhu Hassan, imewakumbuka sana wanawake ndio sababu tamasha hili kuanzishwa huku tukiamini baada ya hapo tutapata mageuzi na kuona wapi tunaanzia wapi kusaidia michezo ya wanawake kuifanga iwe juu na kupewa kipaumbele," alisema Dk. Hassan.

## Malima aitaka TOC kushiriki Olimpiki

Na Oscar Assenga, TANGA

MKUU wa Mkoa wa Tanga, Adam Malima ameitaka Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC) kuhakikisha wanajiwekea malengo makubwa ya kuhakikisha timu ya Mpira wa Magongo inashiriki mashindano ya Olimpiki mwaka 2024.

Malima aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo ya walimu wa mchezo wa pira wa Magongo yaliyoanza Septemba 15 hapa Tanga kwenye Ukumbi wa Hoteli ya Nyumbani.

Mafunzo hayo wamewashirikisha washiriki kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara na Visiwani yakiratibiwa na TOC na Chama cha Mpira wa Magongo Tanzania THA.

Alisema watengeneze malengo ya lazima na wajiwekee malengo makubwa yatakayokuwa na tija siku za usoni kwa kuhakikisha wanashiriki mashindano makubwa na wanafanya vizuri.

"Ndugu zangu tuwe na malengo makubwa ya kushiriki mashindano ya Olimpiki mwaka 2024," alisema Malima.

# LYANGA AREJEA AZAM KUIVAA HORSEED

Na Adam Fungamwango

WINGA machachari wa Azam FC, ambaye aliumia kwenye mechi ya mkondo wa kwanza wa michuano ya Kombe la Shirikisho hatua ya awali, Ayoub Lyanga, amepona na sasa atacheza kwenye mechi ya marudiano Jumamosi, kwenye Uwanja wa Uhuru, jijini Dar es Salaam.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Thabit Zacharia amesema, kuwa Lyanga ambaye alifunga bao la kwanza kwenye mechi ya kwanza, Azam ikishinda mabao 3-1, kwenye Uwanja wa Azam Complex, amepona majeraha yake baada ya kuumia kwenye mechi hiyo na ameanza mazoezi na wenzake kujiandaa na mechi hiyo.

"Alipata majeraha kwenye mechi hiyo, lakini sasa yuko fiti kuivaa Horseed. Ila mchezaji ambaye aliikosa mechi hiyo Charles Zulu, ataendelea kuikosa kutokana na matatizo ya nyaraka, pamoja na yeye pia kuwa majeruhi," alisema.

Zulu ambaye ni raia wa Zambia, ni mmoja wa wachezaji waliosajiliwa msimu huu kutoka Cape Town City ya Afrika Kusini.

Kuhusu mechi ya Jumamosi, Zacharia alisema kuwa, mazoezi yanaendelea vizuri na kuongeza kuwa wapinzani wao si timu ya kubeza, hivyo wataingia kwa tahadhari kukabiliana nao, ikiwa ni pamoja na kuulinda ushindi walioupata.

"Tuko mbele kwa mabao mawili. Tutakachofanya kwenye mechi hiyo ni kulinda zaidi ushindi wetu, kwa sababu hata wao wanahitaji mabao 2-0, ili wasonge mbele. Tunalijua hilo na tutapambana," alisema.

Mechi hiyo itarudiwa nchini Tanzania kwenye Uwanja wa Uhuru, kutokana na kutokuwa na usalama wa kuridhisha nchini Somalia.




Wanamuziki wa bendi ya Waluguru Original 'wakishambulia' jukwaa kwenye moja ya maonyesho yao, mjini Morogoro. PICHA: SABATO KASIKA

# Waluguru Original kukinukisha Arusha

Na Sabato Kasika

BENDI ya Waluguru Original ya mjini Morogoro, imelazimika kufanya mazoezi mfululizo tangu mwanzo wa mwezi huu ikiwa ni maandalizi ya kutoa burudani kwenye onyesho maalum liitwalo 'Usiku wa Wafia Dansi'.

Naye Mkurugenzi wa bendi hiyo, Killer Boy alisema wanamuziki wake wanajifua mazoezini kila siku, ili kuhakikisha siku ya onyesho hilo kikosi hicho kinaonyesha uwezo wake wa kutoa burudani.

"Tunafanya mazoezi kila siku, kwa ajili ya kujiweka sawa, ili Usiku wa Wafia Dansi tutoe burudani kali, pia tunaendelea kutoa burudani katika maonyesho ya mwisho wa wiki," alisema Killer.

Killer alisema, onyesho hilo litafanyika mwishoni mwa mwezi huu, jijini Arusha likiwa ni la pili kwa mwaka huu na kwamba, la kwanza lilifanyika mwezi Mei mjini Morogoro likishirikisha bendi mbalimbali.

"Bendi yetu ilishiriki kwa mara ya kwanza katika onyesho hilo la Morogoro na tulipata uzoefu kwamba kuna haja ya kujinoa zaidi, ndiyo maana tunaendelea na mazoezi tukijiandaa, kwa ajili ya onyesho hilo, litakalofanyika Arusha," alisema.

Kwa upande wake mratibu wa onyesho hilo Benard James alisema, litashirikisha bendi tatu za muziki wa dansi za Waluguru Original, Bogos Musica ya jijini Dar es Salaam na Mjengoni Classic ya jijini Arusha.

Michezo

Ijumaa Septemba 17, 2021
Nipashe



Simeone: Griezmann atarudi kwenye ubora UKURASA 20



Nyota wa Paris St Germain, Lionel Messi (katikati), akijaribu kuwatoka walinzi wa Club Brugge katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya wa kundi A dhidi ya timu hizo, juzi Jumatano kwenye Uwanja wa Jan Breydel mjini Bruges nchini Ubelgiji. Timu hizo zilitoka sare ya 1-1. **PICHA: MTANDAO**

# GOMEZ: SIMBA IPO TAYARI KWA MIKIKI

## Yatua Dar leo tayari kuivaa TP Mazembe, kambi yaleta mafanikio makubwa huku...

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI Simba ikitarajiwa kuwasili leo jijini Dar es Salaam ikitokea mkoani Arusha, kocha wa timu hiyo, Didier Gomez amesema kikosi chake kipo tayari kwa mikiki ya Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya kimataifa.

Simba wanawasili leo saa saba mchana tayari kwa mchezo wao wa kirafiki dhidi ya TP Mazembe kwenye maadhimisho ya kilele cha Wiki ya Simba (Simba Day).

Gomez akizungumza na gazeti hili jana muda mfupi baada ya mazoezi ya asubuhi, alisema kambi yake ya mkoani Arusha imefanikiwa kwa asilimia kubwa na sasa wanakuja Dar es Salaam wakiwa sawa kwa asilimia kubwa.

"Michezo miwili ya kirafiki tuliyocheza huku imetuonyesha wapi tulipo kwa sasa, tunarejea Dar es Salaam kwa ajili ya mchezo wetu na TP Mazembe pamoja na maandalizi ya mwisho mwisho kuelekea kwenye Ligi Kuu, nashukuru tulichokuwa tunakitaka kwenye kambi tumefanikiwa kukipata," alisema Gomez.

Alisema mchezo dhidi ya Mazembe nao utakuwa kipimo kizuri na aliwapa hamasa mashabiki wa timu hiyo kujitokeza kwa wingi kwenye mchezo huo ikiwa ni siku yao maalum.

**MAZEMBE KUTUA KESHO**

Katika hatua nyingine,TP Mazembe wanatarajiwa kutua nchini kesho saa saba mchana wakiwa na kikosi kamili tayari kwa mchezo huo wa Simba Day.

Kaimu Ofisa Habari wa klabu hiyo, Ezekiel Kamwaga, alisema timu hiyo imesogezewa mbele mchezo wao wa Ligi Kuu nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kwa wiki moja ili kutoa nafasi kwao ya kuumana na Simba kwenye tamasha la 'Simba Day'.

"Mazembe tayari wametupa uthibitisho rasmi wa kutua kesho mchana, awali walikuwa na mchezo wa ligi siku hiyo ya Septemba 19, lakini kwa kutambua ukubwa wa Simba na ushirikiano mzuri uliopo baina ya timu hizi, waliomba kwa shirikisho lao la soka kusogezwa mbele na imekuwa hivyo," alisema Kamwaga.

Alisema kuwa makocha wa timu zote mbili watakutana na waandishi wa habari kesho saa tisa alasili kwa ajili ya kuzungumzia maandalizi yao kiufundi kuelekea kwenye mchezo huo.

**YAZINDUA MASCOT**

wametambulisha Mascot rasmi wa klabu hiyo watakaojulikana kama Mo rafiki kwa lengo la kuongeza hamasa pindi timu iwapo uwanjani kwenye mechi mbalimbali kuanzia msimu 2021/22.

Kupitia kurasa zao za mitandao ya kijamii klabu hiyo ya Simba wameandika kuwa: "Atakuwepo kwenye michezo yetu na kwa kuanzia utakutana nae siku ya Simba Day."

# Yanga yapaa na matumaini kibao

**Na Tunu Hasaan, (TUDARCo)**

TIMU ya Yanga leo inapaa kuelekea nchini Nigeria ikiwa na matumaini makubwa ya kupindua matokeo ili kusonga mbele kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya wapinzani wao Rivers United.

Yanga itashuka dimbani Jumapili kwenye mchezo huo wa marudiano hatua ya awali ya mashindano hayo makubwa zaidi kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

Wanakwenda kwenye mchezo huo, huku wakiwa na kumbukumbu mbaya ya kupoteza kwa kufungwa 1-0 katika dimba la Benjamin Mkapa Jumapili iliyopita, hivyo wanahitaji angalau ushindi wa 2-0, ili kusonga mbele.

Akizungumza na gazeti hili jana Ofisa Habari wa klabu ya Yanga, Hassan Bumbuli alisema kikosi kipo salama na waliendelea na mazoezi juzi na jana asubuhi na mchana walifanikiwa kufanya vipimo vya ugonjwa wa COVID-19 kwa wachezaji, benchi la ufundi na viongozi wote.

"Kila kitu kipo vizuri na wachezaji wapo sawa, kwa wale walioonekana kuwa majeruhi baada ya mchezo wa kwanza, nao walifanya mazoezi pamoja na wengine na hivyo kwa sasa wako fiti," alisema Bumbuli.

Alisema wachezaji ambao watakuwa tayari kwa ajili ya mchezo huo ni 22 ukiacha wale majeruhi ambao ni Mapinduzi Balama, David Brayson na Yassin Mustafa.

"Wachezaji ambao hawatakuwapo ni Fiston Mayele, Khaleed Aucho na Djuma Shaban ambao wana utata na ITC, ingawa watakuwa sehemu ya msafara wetu," alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31

9 770856 541002 >